

NJIA YA UZIMA



Asante, Ndugu Borders.

² Mwajua, ni majaliwa mazuri sana kuwa miongoni mwa watu, na halafu kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza katika sinagogi la Kiyahudi, ni jambo adimu sana kwangu. Halafu basi, kufahamu jambo hili zaidi, utaratibu hapa wa... wa haya Magombo, na jinsi yanavyoshughulikiwa, na kadhalika, ungekuwa ni wakati mzuri kuja wakati mwingine na kufanya ibada ya uponyaji katika sinagogi hili, na kuwafanya Wa—Wayahudi, na... [Ndugu mmoja anasema, “Njoo. Umekaribishwa, Ndugu Branham. Njoo.”—Mh.] Asante, Ndugu. Asante, sana.

³ Daima nimewahurumia Wayahudi, labda hakuna yeyote hapa, lakini, asubuhi ya leo, lakini ninawahurumia, daima nimewahurumia. Nami ninaamini ya kwamba siku moja Kanisa la—la Mataifa litaupeleka Ujumbe kwa Myahudi, kama vile Myahudi alivyompa Mataifa. Ninaamini hilo kwa moyo wangu wote. Ndipo basi Huo utakapomrudia Myahudi kikamilifu, angalieni, mlango wa Mataifa utafungwa wakati huo, na itakuwa ni Myahudi, kwa hiyo sasa ndio wakati. Nina furaha sana kuwa ndani sasa hivi, upande wa ndani.

⁴ Mungu ambariki maskini mtu huyu mwenye neema, Ndugu Michaelson. Sijawahi kumwona maishani mwangu, nisingemtambua kama angalikuwa amesimama hapa. Huenda akawa kwenye wasikilizaji, nami nisingejua hilo. Lakini nimesikia kipindi chake, nami ninakithamini, mtumishi mashuhuri wa Mungu, maskini Myahudi huyo ambaye ameyatoa maisha yake, sasa, katika utumishi wa Mungu. Mimi...na kwa...Ninapenda jinsi anavyolisema hilo, “Yesu wangu.” Naam, “Yesu wangu.” Nafikiri hilo lilikuwa ni jambo la kushangaza sana kwa Myahudi kusema hivyo.

⁵ Hakika amekuwa kinaru wa mwenge, mshika mwenge kwa ajili ya Wayahudi katika nchi hii, kote Marekani hapa. Na maombi yangu maaminifu ni: Mungu, aipe maskini mikono hiyo mikongwe nguvu za kuushikilia mpaka Yesu atakapokuja, ikiwezekana. Ninampenda. Ninawapenda wazee walipopigana vita vizuri.

⁶ Kumbukeni Dk. F. F. Bosworth, mmoja wa wenzangu, nilipoingia kumwona, alikuwa na umri wa miaka themanini na minne, alikuwa ameinyoosha maskini mikono yake namna *hiyo*. Nao, huko nyuma, ndio kwanza watoke kwenye huduma za Afrika akiwa na umri wa miaka themanini, akifanya umishenari pamoja nami huko msituni. Nami nikamkimbililia na kumkumbatia kwa mikono yangu, nilijua alikuwa yuafa,

nami nikalia tu, “Baba yangu, baba yangu, magari ya Israeli na wapanda farasi wake!” Mtu hodari namna hiyo.

Naye akasema, “Huu ndio wakati wa furaha sana maishani mwangu, Ndugu Branham,” akasema.

Nikasema, “Unajua unakufa?”

⁷ Akasema, “Siwezi kufa, tayari nimekuwa mfu kwa miaka sitini.” Akasema, “Mimi . . .” Akasema, “Ninangojea tu wakati nitakapoona yale yote niliyoishia, nimwone Yeye akiingia kwenye mlango ule kunikaribisha Nyumbani Mwake.”

Kisha kasema, “Hiyo ndiyo njia.”

Ninawazia basi:

Maisha ya watu mashuhuri yote
yanatukumbusha
Tunaweza kuyafanya maisha yetu adhimu,
Tunapoachana, tunaacha nyuma yetu
Kumbukumbu za kudumu;

⁸ Ni kweli. [Ndugu Kopp anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Naam? [Anaendelea kuzungumza.] Hu—huenda sikusikia ninii tu. . . Nilisikia ya kwamba alipeana mikono na. . . akisimama chumbani, akitikisa. . . [Anaendelea kuzungumza.] Naam, Bwana. Naam. Naam. Naam, Bwana. Hilo, nilisikia hilo. Hiyo ni sawa, Ndugu Kopp, nina furaha kwamba ulinikumbusha juu ya. . . Naam.

⁹ Walisema kitambo sana kabla hajafa, ama, kwenda Nyumbani, alisimama, na, kupeana mikono na waongofu wake waliomjia Kristo kupitia huduma yake kwa muda mrefu, kisha akakata roho, akaenda kuwa pamoja nao. Ni hodari jinsi gani! Ninapenda tu vitu kama hivyo. Hiyo ni ninii tu. . .

¹⁰ Ndugu, ni majaliwa makubwa sana kuwa hapa Los Angeles, ama, Lango hili la Kusini, chochote panachoweza kuitwa hapa, ambapo tunafanya mkutano na ushirika huu mzuri. Ni. . . Mnalianika humu ndani, wala ni—nisingekuja kama sikuwa na namna fulani ya mvuto wa kuja.

¹¹ Nami ninatambua ya kwamba—ya kwamba huduma yangu imekuwa mahali ambapo karibu imefikia kwenye shindano la kuamua, Mimi. . . kama vile vitu vyote vinafikia ambapo. . . mimi. . . wameanza kunea mambo, ulimwengu umeanza, na mashirika, na kadhalika, kwamba mimi ni nabii wa uongo, na—na kila kitu, nami ninatazamia hilo kuja, mimi. . . ni ajabu halikuwa limekuja kabla ya sasa, na, bali ninalitarajia liwe baya zaidi.

¹² Na kuona kwamba katika saa hii ya majaribu yangu, na huku nikipitia kwenye fadhaa kuu, kwamba ninyi ndugu mnafungua mikono yenu, nami ninawathamini. Bwana awabariki. Nami nipo hapa kufanya kila nijuacho kufanya, ku—kuyasaidia makanisa yenu kuwa na nguvu zaidi, kuunganisha udugu

pamoja katika moyo mmoja, na hilo ndilo kusudi nililo nalo. Na, kama nilivyosema jana usiku, kuvuta juya kila kona ndogo na kushika kila samaki mdogo wa mtoni awezaye kushikwa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

¹³ Na sasa, jana usiku nilichelewa, nasi tulianza tumechelewa. Nami karibu kila mara huchelewa, mama yangu alisema nilikuwa mtoto mchanga wa miezi tisa kamili, na kwa namna fulani nilichelewa kufika hapa. Nami nilizaliwa nikiwa na uzito wa ratili tano tu, nami nilikuwa na mwanzo mbaya, wala kamwe sikupata kuwa mkubwa sana. Nami ninaninii tu. . . Nilichelewa kwenye arusi yangu, ni—nilimfanya mke wangu kungojea kwa muda mrefu. Na sikuzote ni kungoja na kuchelewa. Sasa, laiti ningeweza tu kuchelewa kwenye mazishi yangu, hivyo tu. Hivyo tu. Niwaache tu wangoje kadiri wawezavyo, maana ni—ninataka kuninii tu, maadamu ninaweza kuhubiri Injili, na kushirikiana na ndugu zangu. Na sasa, jinsi. . . Nitajaribu kuharakisha kidogo zaidi usiku wa leo.

¹⁴ Jana usiku. . . Sasa, ni wahudumu tu hapa kama ninavyosikia. Ninajaribu kuweka chambo. Sasa, kuna wenye dhambi wanaoketi huko nje, mnaona. Na jambo la kwanza. . . Huenda mlishangaa ni kwa nini sikutoa wito wa madhabahuni. Jambo la kwanza, nilihisi kwamba nilikuwa nimechelewa kidogo tu, na hilo huwachosha watu, na kadhalika. Lakini chambo kidogo tu chini ya upambanuzi ama kitu fulani, na hiyo itafanya ninii zao. . . itawavutia. Kisha unatandaza wavu wako kote, unaona, kisha uwaingize ndani. Ni—nivumilieni tu sasa, ninaenda tu jinsi ninavyowazia Roho ananiongoza kwenda.

¹⁵ Na sasa, kama tukiingiza wengine kwenye jarife wanaotaka kuokolewa na kujazwa na Roho Mtakatifu, ndugu, mnajua wanatoka wilaya gani, wapelekeni kanisani mwenu, maana hiyo. . . kuwavuta tu madhabahuni ndio umbali tu tuwezao kuwafikisha kule, na, ndipo unawapeleka sehemu iliyosalia kutoka hapo. Waingizeni ndani, na muwabatize, kisha mkae nao mpaka watakapompokea Roho Mtakatifu. Na—na hilo ndilo lililotuleta hapa katika saa hii kuu yenye giza, kama vile jua linavyotua magharibi, na Nuru ya jioni imekwisha.

¹⁶ Nami. . . Miongoni mwa watu. . . Kama ninyi, wengi wenu, si siri, nyote mna kanda zangu, ninyi nyote, na, lakini miongoni mwa watu huko nje, kamwe siyaendei Mafundisho magumu ya Kimaandiko, kama vile ningetaka kama ningalikuwa maskanini ama chochote kile, na—na kwenye kanda ambapo wahudumu wangeweza kuzichukua na kuzisoma.

¹⁷ Nami nimekuja asubuhi ya leo pamoja na Myunani mmoja kutoka nchi ya kale, naye ana kanda zangu za saa sita juu ya *Neno Mbegu*. Naye ananiambia ya kwamba yeye huenda tu kidogo kila siku, na kuchukua hayo, na kuyavunja, na kuyaingiza katika Kiyunani, na jinsi alivyokuwa akionyesha

jinsi (Pasipo mimi kujua chochote juu yake.), jinsi yanavyokaa pamoja namna hiyo. Hizo ni kwa ajili ya kujifunza, hapa ndani tunajaribu kuvua samaki. Jambo ndilo hili: Tunaweka chambo huko nje. wala kamwe hatumwonyeshi samaki ndoana, unamwonyesha chambo, yeye ananyakua chambo na kunaswa na ndoana.

¹⁸ Kwa hiyo huo—kwa hiyo huo ndio wakati wangu wote katika kuwaombea wagonjwa na kadhalika, ni kuvutia tu jicho la mwenye dhambi, hicho ndicho chambo, lakini ndoana, ndoana ya Injili, wewe tumia hiyo. Nitatikisa tu chambo mbele yake, mnaona, kusudi m—mtumie ndoana.

¹⁹ Kwa hiyo basi. . . Na, usiku wa leo, nitajaribu kufanya ninii yangu. . . mazungumzo yetu madogo yawe mafupi zaidi, mwajua, kusudi niweze tu. . . Naye Ndugu Borders huzungumza kidogo kabla sijafanya hivyo, na—na kuingia. Nitajaribu kutoa hotuba zangu, ama, maskini mazungumzo ya utotoni kwenu ninyi ndugu. Na—na kama ungewazia jambo hilo. . . Bila shaka jambo lolote ningeweza kusema labda lingekuwa ni la kitoto kwenu, lakini, ninyi nyote ni waalimu, nami si mwalimu. Nami. . . Lakini kusudi langu ni kujaribu kususaidia Ufalme wa Mungu, kujaribu kuyaimarisha makanisa yenu, na kuimarisha udugu miongoni mwa wanadamu, tunapokungojea Kuja kwa Bwana. Nami nina hakika mtaelewa hilo.

²⁰ Na sasa, hii hapa, Los Angeles, kama nilivyoona asubuhi ya leo, na kukutana na ninii yangu, baadhi ya marafiki zangu hapa: Ndugu Sothmann *pale* kutoka Jeffersonville, asili yake ni Mkanada; naye Ndugu Tom pia ni Mkanada, ambaye anaishi pamoja nasi huko Jeffersonville wakati huu; na—na Ndugu Welch Evans *pale* kutoka Tifton, Georgia, pia ni mgeni pamoja nasi, akiendesha gari maili elfu moja mia tano kila Jumapili kuninii. . . ili, kunisikia nikihubiri Injili. Sasa, pia yule *pale* Ndugu Norman kutoka. . . na Dada Norman, na Dada Evans, na Ndugu Willie, siwezi kamwe kuwazia. . . Lile kundi dogo linaloketi kwenye msongamano mdogo *pale*, ambao wamekuja hapa pamoja nasi, na kuomba pamoja nasi, na kutuimarisha tunapoingia, kwa ajili ya ibada. Nina furaha kuwa nao pamoja nasi mikutanoni.

²¹ Sasa, katika kuandaa mkutano huu, ni—niliangalia, nasi tulikuwa na kitabu cha mikutano, watu tu. Na shida tuliyo nayo sasa, kati ya ndugu wa kimadhehebu, na wengi wao, wao, ndugu wa kimadhehebu, jinsi ninyi nyote mlivyo, hata hivyo, ningetaka kuninii, juu ya mimbara hii asubuhi ya leo, kutoa maoni yangu, mnaona. Ninii. . . Mnajua wenyewe, ndugu, miongoni mwa watu wenu mnaweza kusema jambo fulani *hivi*, na mmoja atalichukua *hivi* na kuanza kuliegemeza *hivi*, naye atamwambia huyo mwingine, huyo mwingine kwa anayefuata, muda si muda mwajua, yote yamevurugika. Na mmoja ataegemea upande *huu*, na kulichukua upande *mwingine*, mnajua hilo.

22 Nami nina hakika ya kwamba ninyi ndugu mnaelewa ya kwamba hivyo ndivyo mambo mengi yanavyosemwa kunihusu mimi, hata yanachukuliwa tu na wengine na kueleweka vibaya, na kupotoshwa, si maana yake hata kidogo.

23 Kuhusu kulipinga dhehebu, bila shaka sivyo, ndugu zangu wako mle. Ni kama tu, kuna watu wengi kupita kiasi, siku hizi, wanaotegemea madhehebu. Sasa, tuna ndugu aliyeketi hapa kutoka kanisa la United Brethren, na mahali mbalimbali, ni . . . madhehebu hayo ni sawa, mradi tu unanyoosha ushoroba mbele kidogo, unaweza kulifungua lango, na kunywea kwenye kisima cha tatu, mnajua ninalomaanisha, ambacho Yakobo alichimba, na—na unaweza kufanya ushirika.

24 Lakini unapokuja, “Mradi tu wewe ni mfuasi wa dhehebu, hilo ndilo lote likupasalo kufanya,” la, kuna mengi zaidi ya hayo kwake, ndugu. Na hapo ndipo ulimwengu mzima umenini daima. . . Nanyi. . . Tuna mwanahistoria mzuri ameketi hapa pamoja nasi asubuhi ya leo, nasi tunajua ya kwamba makanisa, mara yanapochora mstari huo, dhehebu, “Sisi *ndio*,” papo hapo Mungu huwaacha, nao wanakufa wala hawafufuki tena. Mnaona? Hakuna historia ya mahali ambapo kanisa liliwahi kuanguka, na likawahi kuinuka tena, haliinuki. Na kwa sababu. . .

25 Wakati nilipoingia katika jambo hili kwa mara ya kwanza, katika huduma hii, ilikuwa ni ninyi ndugu wa kanisa la United Pentecostal mlionikaribisha kwanza. Huyu alikuwa ni Ndugu Richard Reed, Ndugu Jack Moore, na Ndugu Ben Pemberton ambaye. . . na St. Louis, mkutano wangu wa kwanza. Nao mkutano wa kwanza niliowahi kuhudhuria ulikuwa, na niliojua lolote kuhusu. . . ulikuwa ni P. A. ya W. na P. A. ya J. C., kama walivyokuwa, kabla hawajaungana na kuja pamoja, Ndugu Ryall huko Mishawaka. Wala sijawahi kuona ushirika mzuri kama huo wa ndugu.

26 Vema, basi, nikakuta. . . Nilifikiri hivyo ndivyo Pentekoste yote ilivyokuwa, ya kwamba hiyo ilikuwa ndiyo Pentekoste, lakini nikaona kulikuwako na makundi mbalimbali kote kila mahali, na kulikuwa na watu wazuri katika kila moja yao. Kwa hiyo, nimejaribu kusimama kwenye pengo huku nimeinua mikono yangu, nikijaribu kumwita kila ndugu kwenye umoja wa ushirika, ili tuweze kuwa na ufahamu, haidhuru wanaamini nini, maadamu sisi ni ndugu. Kwa sababu nina hakika kama ningejitokea mwenyewe. . . Kuna dosari nyingi sana ambazo Mungu angeweza kuelekezea kidole Chake usoni mwangu asubuhi ya leo, na kusema, “Kijana, wewe mwenyewe uko mbali na kukamilika.” Kwa hiyo hivyo ndivyo nimejaribu kujisikia kuhusu kila mtu, kuwavuta pamoja. Sasa, hilo ndilo kusudi langu, ni kufanya ushirika wa muungano. Mungu awabariki daima.

27 Na katika, kama nilivyoanza kusema dakika chache zilizopita, katikati ya haya yote, hata hivyo kulikuwa na mamia ya mahali panapoita, pia kutoka kwenye maeneo ya umishenari, na sasa, nina safari ya kiinjalisti, ninavuka nchi, na punde tu nitakapoondoka huko, ninaenda katika nchi za kigeni kwenye ziara ya kimishenari.

28 Nami ninajaribu nafsini mwangu, ambalo sina wakati wa kueleza, kutafuta jambo fulani kutoka kwa Mungu, kwa sababu ninaamini ya kwamba kule kukaribi- . . . kuja kwa Kristo kumekaribia kuliko tunavyota- . . . tunavyowazia. Ninaamini kuko moja kwa moja mlangoni, na kweli linanitia wasiwasi ninapoliwazia, si wasiwasi kwa ajili yangu mwenyewe, lakini wasiwasi juu ya hili: Je, nimefanya vizuri sana niwezavyo? Je, kuna wakia moja zaidi ndani yangu ambayo ningeweza kutoa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu? Kuna kitu ambacho ningeweza kufanya? Kwa sababu hii ndiyo nafasi pekee tutakayopata kuwa nayo, sasa hivi.

29 Nami nime—nimelikemea Kanisa, nimewakemea watu wetu, nimewakemea dada zetu kwa kukata nywele zao, nikawakemea kwa kujipodoa, nimewakemea ndugu zetu kwa kuwaruhusu kufanya hivyo, na wahudumu wetu na mambo kama hayo, si kwa sababu nina lolote dhidi yao, ni kwa sababu kwamba nina—ninawaonea wivu, wao ni urithi wa Mungu.

30 Nami—nami nimewakemea ndugu zangu wahudumu kwa kutoninii. . . kwa kujivuta tu katika kitu kimoja kidogo katika kundi. Sasa, ningefikiri kama kulikuwako na dhehebu ambalo lingesema, “Tunaamini *hili*, koma, pamoja na yote ambayo Mungu anaweza kuongezea kwake,” lakini tunapofanya milki yetu ya kimadhehebu, tunasema, “Tunaamini *hili*, basi,” naye Roho Mtakatifu anaingia moja kwa moja ndani, na kuondoka moja kwa moja ndani yake, hiyo ni kweli, mnaona. Sasa, kama tunaweza kulimalizia kwa koma, basi tunaendelea tu kukua.

31 Hivi majuzi, nilikuwa na m—mkutano pamoja na ndugu wa Kilutheri, nadhani nyote mlisikia habari zake, huko Minneapolis, Minnesota. Na loo, jamani, jinsi kweli alinikosoa vikali katika barua ya kurasa ishirini na mbili! Akasema, “Wazo lenyewe!” Kasema, “Niliendesha gari maili kumi na tano jana usiku, kupitia dhoruba ya theluji mbaya sana, nikifikiri ningemsikia mtumishi wa Kristo, nami nilisikia nini, ila mpiga ramli aliyepigwa msasa.” Na loo, yeye. . . Kisha kasema, “Wazo lenyewe la wewe, mtu mwenye miaka kumi na mitano katika huduma ya umishenari, halafu—halafu kusema umekuwa ukihubiri Injili kwa miaka ishirini na mitano,” na kusema, “kisha kusikia. . . kukusikia ukitumia sarufi unayotumia, na—na Fundisho lenyewe unalo—unalonena,” akasema, “hata ulisema mengi sana jana usiku kwamba Shetani asingeweza kuponya.” Kasema, “Jionee aibu kwa tamshi kama hilo.”

Nami nikawaza, “Mshauri wa chuo cha Kilutheri.”

³² Kisha akasema, “Papa hapa sio mbali na chuo chetu hapa, kuna mwanamke aliye na pepo. Yeye huvaa aproni kubwa, naye watu wanaingia, naye anawawekea mi—mikono. Ndipo naye anavuta mishipa yao ya damu, na kuchukua nywele chache kutoka nyuma ya shingo yake, na kuzikunja, anatoa damu mle, kisha anashuka kwenye kijito nyuma yake, na kuzitupa juu ya kichwa chake namna *hiyo* kwenye kijito, anaanza kutembea huku mikono yake. . . .”

³³ Kisha kasema, “Watu wanaosimama hapo, kama ikimbidi kuangalia nyuma, huo ugonjwa uko kwenye damu ya mtu aliye kwenye nywele zake,” kisha kasema, “basi wakati, akiangalia nyuma, huo ugonjwa utamrudia huyo mtu, lakini kama sivyo,” kasema, “huyo mtu atapata afya.” Kisha kasema, “Karibu asilimia ishirini ya hao hupata afya. Halafu unasema ati ibilisi hawezi kuponya.”

³⁴ Loo, a—alikuwa na mtazamo mzuri wa kiakili, lakini, ndugu, hilo silo tunaloenda, si kiakili, tunayaenda Maandiko. Kwa hiyo ni—nikawazia tu, “Vema, barua ya kurasa ishirini na mbili. . . .” Hata hakunitambulisha kama “Ndugu,” alisema tu, “Branham.” Kwa hiyo nikawaza, “Vema. . . .”

Akasema, “Nawe ukizungumza juu ya miaka yako,” kasema, “nilikuwa nikihubiri Injili kabla hujazaliwa.”

³⁵ “Vema,” nikawazia, “mtu ambaye amehubiri Injili kwa muda mrefu hivyo anapaswa kuheshimiwa, haidhuru yeye ni nani.” Mnaona? Tunapaswa kumheshimu. Kwa hiyo nikaketi chini na kumwandikia, maskini mkwaruzo wangu, vizuri sana nilivyoweza, kurasa mbili kumjibu, kumtambua. Nami ni—nikasema, “Ndugu mpendwa, hakika ninathamini miaka mingi ambayo umetumia na yote haya,” Nikasema, “Ni—ninaithamini, mtumishi wa Kristo. Nami ninauthamini huo ukosoaji.” Sasa, mtu asiyeweza kustahimili ukosoaji, ujuzi wake una kasoro, mnaona, maana Mungu hututumia ukosoaji apate kutusahihisha, kutufanya tuone mambo ye—yetu mbaya. Nimesaidiwa sana na ukosoaji, ambao ni ukosoaji wa kirafiki, bora usiwe tu na chuki, na hasira, bali u—ukosoaji tu wa kirafiki. Kwa hiyo nikasema, “Ninathamini jambo hilo, Bwana.”

³⁶ Ndipo basi nikasema, “Lakini jambo moja tu ningetaka kuelezea hapa, kama vile wewe, ukizungumza juu ya sarufi yangu, bila shaka mimi si. . . .Sina elimu, hiyo ni kweli, lakini,” nikasema, “jambo linalonishangaza, kwamba mshauri wa chuo cha Kilutheri angeweka theolojia yake msingi juu ya ujuzi fulani, badala ya Neno la Mungu, ulipozungumza juu ya mchawi ambaye angeweza kuponya.”

³⁷ Nikasema, “Yesu alisema, ‘Kama Shetani anaweza kumtoa Shetani, basi ufalme wake umegawanyika,’ hawezi kuponya. Sasa, unaweza. . . .” Mnaona? “Kama anaweza. . . .Yesu alisema

asingeweza kuponya, nawe ukasema angeweza kuponya. Nitamwamini Yesu,” mnaona, hiyo ni kweli, “kwa sababu Yeye alisema neno la kila mtu na liwe uongo na Lake liwe kweli,” nami nikasema, “Ninamwamini Yesu. Na jambo la kushangaza kwangu, kwamba mshauri wa chuo cha Kilutheri angewekea msingi theolojia yake juu ya . . . ujuzi, ama mhemuko, badala ya Neno la Mungu.” Nikasema, “Mshauri, ama mtu yeyote mwingine, mhudumu yeyote anapaswa kuiwekea theolojia yake msingi juu ya Neno la Bwana.”

³⁸ Pia nikasema, “Bila shaka mimi . . . Na kile unachoita mpiga ramli,” Nikasema, “Nadhani ilikuwa ni ule upambanuzi.” Basi nikasema, “Je, ulijua ya kwamba Mafarisayo na Masadukayo wakati mmoja walitoa tamshi hilo wenyewe, walipoona jambo lile lile likifanywa na Bwana wetu, wakamwita Beelzebuli?” Nikasema, “Sasa, labda, vipi kama niko sahihi? Sasa, Yesu alisema, ‘Roho Mtakatifu atakapokuja kufanya jambo lile lile, kwamba kunena neno dhidi Yake hakutasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala ulimwengu ujao,’ miaka yako hamsini ya kuhubiri haijalishi, neno moja dhidi ya Roho Mtakatifu.” Nikasema, “Ninakusamehe hilo, nami ninajua ya kwamba Mungu atafanya hivyo, kwa kuwa aliona ya kwamba hukulielewa.” Basi nikamwandikia barua nzuri sana nilivyoweza. Baadaye nikapata ba—barua ya kunialika kuja huku.

³⁹ Kwa hiyo, [Ndugu Branham anakohoa—Mh.] Nilikuwa na . . . (Samahani.) Nilikuwa na ki—kiamshakinywa cha Wafanyabiashara kule juu, nami nilikuwa nikizungumza kwa niaba ya Wafanyabiashara wa Full Gospel. Ndipo Bw. Moore, Ndugu Jack Moore, wengi wenu ninyi ndugu mnamfhamu, mtu mmoja mzuri, nami . . . yeye . . . huyu Dk. Hegre a—akamjia Ndugu Moore, na kumwuliza kama ningeweza . . . kama angenileta chuoni.

⁴⁰ Nikawaza, “Hakika nitalijutia sasa.” Kwa hiyo mimi . . . Ndugu Moore ni mwanatheolojia, kwa hiyo nikawazia, “Vema, afadhali niende pamoja naye.” Na kwa hiyo nikasema, “Wewe keti papo hapo karibu nami, ndipo akiongea maneno na sarufi nisizoelewa, nitakupiga teke mguuni namna *hiyo*, nawe uchukue kuanzia hapo na kuendelea.”

Naye akasema, “Vema.”

⁴¹ Kwa hiyo tukaenda chuoni. Basi tulipofika kule, walikuwa na mahali karibu, ukubwa wa ukumbi huu hapa kwa ajili ya cha—chakula cha kutwa. Na ninii . . . ilikuwa ni Wanorwe, nao walikuwa wameandaa chakula chao cha kutwa, na kizuri sana, kitamu. Naye huyo mshauri akaketi upande mmoja, na mwenzake upande mwingine.

Kwa hiyo, baada ya mimi kumaliza, akasema, “Ndugu Branham, tunataka kukuuliza maswali kadhaa.”

42 Nikasema, “Hebu kwanza kidogo niseme neno moja.” Nikasema, “Hu—huenda nisiweze kuljibu swali lako,” Nikasema, “Mimi... kama siwezi, itakuwa sawa kama Ndugu Moore atanisaidia hapa.” Nikasema, “Lakini nimeninii... Hu—huenda nisiwe mzuri katika kuyajibu maswali yenu, bali nitafanya niwezayo.”

43 Naye akasema, “Hivi ndivyo ilivyo,” kasema, “tumesikia habari za Wapentekoste, miaka na miaka,” halafu kasema, “tukaenda kuwaona.” Kisha kasema, “Tuliona nini, ila kupiga viti mateke, kuvunja madirisha, na—na kila kitu namna hiyo,” kasema, “na kelele zote tulizowahi kusikia maishani mwetu.” Kasema, “Kwani watu hao wana nini?”

Nikasema, “Roho Mtakatifu.”

Akasema, “Ati Roho Mtakatifu?”

Nikasema, “Naam.” Nikasema... .

Akasema, “Je, wewe umekuwa Mpentekoste sikuzote?”

44 Nikasema, “Vema, wakati mmoja nilikuwa mfuasi wa Kanisa la Baptisti ya Kimishenari nilipokuwa mvulana tu, niliwekwa wakfu, lakini,” nikasema, “mara baada ya kuwekwa wakfu,” nikasema, “ni—nilimpokea Roho Mtakatifu, kwa hiyo nadhani nimekuwa Mpentekoste.”

45 Akasema, “Unataka kuniambia ati hao ni Wapentekoste, hao Wapentekoste, ati huyo ni Roho Mtakatifu anayewafanya wapige viti mateke, na kupiga mayowe namna hiyo?”

46 Nikasema, “Naam, ni Roho Mtakatifu.” Nikasema, “Jambo ni kwamba,” nikasema, “wanapata presha kubwa sana, mvuke, wanaitolea kwenye filimbi badala ya kuitia kwenye injini, kuyafanya magurudumu yafingirike, mnaona, hivyo—hivyo tu.” Nikasema—nikasema, “Hiyo ni kweli.” Nikasema, “Wao... mvuke mwingi sana mle, inawabidi tu kuutoa kwa kupiga filimbi, hayo tu ndiyo nijuayo, mnaona.” Nami nikasema, “Hawawezi kuushikilia zaidi.”

Naye akasema, “Vema... .”

47 Nikasema, “Laiti ningaliweka mafundisho ya kimsingi katika imani ya Kipentekoste, ama imani ya Kipentekoste katika mafundisho ya kimsingi! Hao watu ni watumishi wa Mungu, lakini kwa kweli hawatambui nafasi waliyo nayo, hivyo tu.”

Naye akasema, “Vema, unafikiri sisi Walutheri tuna nini?”

Nikasema, “Roho Mtakatifu.”

Ndipo akasimama, halafu akasema, “Sasa, sijui nikuulize nini.”

48 Nikasema, “Vema, ninasikia ya kwamba kuna kama ekari elfu moja hapa ambazo mumepanda mahindi.” Nikasema, “Kama wanafunzi hawawezi kujilipia, basi wanaweza kufanya kazi chuoni.”

Akasema, “Kweli.”

⁴⁹ Kwa hiyo Bwana akanipa wazo dogo, nami nikasema, “Bwana, wakati mmoja kulikuwa na mtu aliyelima shamba kubwa la...kupanda mahindi, naye akapanda mahindi yake shambani. Basi kesho yake...Asubuhi moja akatoka, ndipo alipoliangalia shamba lake akaona majani mawili madogo.” Mtu yeyote anayekuza mahindi anajua hivyo ndivyo yanavyochipuka, kile tunachoita “mahindi chipukizi” huko Kusini, huchipuka tu namna hiyo, majani mawili madogo.

Ndipo nikasema, “Huyo mtu alisimama kwenye vipandio vya mlango wake, na kusema, ‘Bwana asifiwe kwa ajili ya zao langu la mahindi!’” Nikasema, “Sasa, je, alikuwa na zao la mahindi?”

Akasema, “Vema, a—alikuwa ameanza.”

Nami nikasema, “Vema, kwa uwezekano alikuwa na zao la mahindi.” Mnaona? “Alikuwa nalo katika hali yake ya utotoni.” Nami nikasema, “Hilo lilikuwa nyinyi Walutheri.”

⁵⁰ Ndipo nikasema, “Hatimaye, mahindi hayo yalikuwa yakafikia mahali yakawa na kishada. Nanyi mwajua yale hicho kishada kiliyofanya? Kishada kiliangalia nyuma kwenye majani, na kusema, ‘Sina haja nanyi tena, mimi ni kishada.’ Lakini ilikibidi kutumia hilo jani tena kipate kujizaa tena. Kisha kikatoka kwenye kishada hiki kikaingia kwenye ja—jani, ndipo kikazaa su—suke.”

⁵¹ Nikasema, “Sasa, la kwanza lilikuwa ni wewe Mlutheri, cha pili kilikuwa ni ule mwenendo wa Mungu wa Methodisti, na la tatu, suke, lilikuwa ni lile kundi la Pentekoste lililosababisha kurudishwa kwa karama Kanisani, la ile Punje ya asili iliyoingia ardhini. Ni kurudishwa tu tena, kama alivyosema Yoeli.” Mnaona? Nikasema, “Sasa ninajua tuna kuvu nyingi sana kwenye suke hilo, lakini hata hivyo tuna Punje kidogo mle pia, mwajua.” Nikasema, “Sisi...” Nami nikasema...

Naye akasema, “Vema...”

⁵² Nikasema, “Hiyo ndiyo ile Punje ya asili.” Nikasema, “Sasa, kanisa la Kipentekoste ni kanisa la Kilutheri lililoendelea mbele. Hata hivyo, ninii...kama kusingalikuwako na jani, kusingekuwako na kishada, nao Uhai uliokuwamo katika hilo jani ulifanya kishada, nao Uhai uliokuwa katika kishada ukafanya Punje. Kwa hiyo ni Kanisa lililoendelea la Mungu aliye hai.”

⁵³ Ndipo akasimama, akasukuma sahani yake nyuma, akasema, “Ndugu Branham, nilienda magharibi wakati mmoja. Kwamba yeye...niliandika ninii...Nilisikia kitabu kilichoandikwa juu ya ninii...kuhusu karama zote za kiroho.” Tena kasema, “Ni—nikaenda magharibi kumtafuta mtu huyo,” kisha kasema, “nilipoenda, alisema, ‘Loo, niliandika tu kuzihusu, sikuwa nazo.’ Kasema, ‘Niliandika tu juu yazo.’”

Vema,” kasema, “Ningaliweza kufanya hivyo.” Kisha kasema, “Nilizunguka na kuona haya yote, na nikayaendea makundi ya Kipentekoste na kadhalika,” basi kasema, “Ni—niliwaona wakipaza sauti.”

⁵⁴ Mnaona, ilitokea tu kwamba alikuwa pale, ibilisi alimweka pale wakati usiofaa, mwajua, wakati watu, wakishangilia kweli. Sasa yeye ana maoni, naye akaondoka. Mnaona?

⁵⁵ Ndipo akasema, “Naomba msamaha kwa barua niliyokuandikia.” Kasema, “Nilijiinua kufikia mahali ambapo, hata niliipinga, na hapo ndipo nilipoibania, papo hapo, na kusema hukuwa kitu ila mpiga ramli.” Akasema, “Nakuomba unisamehe.”

Nikasema, “Mbona, bila shaka, Bwana. Kamwe nisingeshikilia chochote, wala kamwe sijafanya hivyo. Unajua niliyokwambia katika ile barua.”

⁵⁶ Akasema, “Nilitaka kusikia kutoka midomoni mwako.” Akasema, “Sasa, Ndugu Branham, kwangu na kwa wanafunzi wote, sote tuna njaa ya Roho Mtakatifu. Tufanyeje?”

⁵⁷ Kwa hiyo mnajua yale niliyomwambia, sivyo? Nilisema, “Geuzeni migongo yenu, migongo yenu *hivi*, na nyuso zenu zielekee ukutani, kote kote, nanyi mkusudie moyoni mwenu ya kwamba humtaondoka magotini mwenu kamwe mpaka Mungu atakapowapa ubatizo wa Roho Mtakatifu.” Kisha nikasema, “Sasa msiwazie jambo *hili*, wala *lile*, wala *linginelo*, kaeni tu hapo na kusema, ‘Mungu, nataka Roho Mtakatifu.’” Nikazunguka na kuwawekea mikono, ndipo arobaini wakampokea Roho Mtakatifu papo hapo. Na sasa wamefikia kama watu mia tano kamili, wakiendelea, wakiwa na ishara, miujiza, na maajabu, na kadhalika. Mnaona?

⁵⁸ Ndugu, ninaamini ya kwamba tunacho Kitu ambacho ulimwengu unapaswa kuwa nacho. Lakini hatuna budi kukiendea kwa njia ambayo . . . Vipi kama ungalikuwa seremala? Hebu mchukue tu mtu aliye hapa mwishoni, ama, Ndugu Borders pale ni seremala, naamini.

⁵⁹ Vema, vipi kama alikuwa akipigilia kwa nyundo namna *hii*, na kuipigilia misumari, nami nilikuwa na nyundo ya namna fulani inayojiendesha ambayo ninaimwagia kopo la misumari, na kuishikilia *hivi*, kisha *rruut*, na kuzipigilia mbao hizo vizuri sana kuliko alivyoweza kwa nyundo yake?

⁶⁰ Sasa, kama nikimwendea, niseme, “Aa, jamani, hata huko ndani yake, hujui lolote kuihusu. Mbona, unaviponda vidole vyako! Jamani, kwanza kabisa huna bidhaa,” Ninamwudhi, kamwe sitaiuza hiyo nyundo. Hiyo ni kweli. Mnaona? Ni jinsi ninavyoenenda na kile nilicho nacho. Bidhaa yangu, najua, ni bora kuliko aliyo nayo, lakini sina budi kukumbuka, sina budi kumwendea kwa njia ifaayo.

Na kama nikimwendea, na kusema, “U hali gani, Bwana? Jina langu ni Branham.”

“Langu ni Borders.”

“Naona wewe ni seremala.”

“Naam. Naam, bwana, ndivyo nilivyo.”

“Kweli ninaamini wewe ni seremala halisi pia.”

“Naam.”

“Nilikuwa nikiangalia jinsi ulivyokuwa ukitumia nyundo yako.”

“Loo, naam, maskini Betsy amekuwa pamoja nami kwa muda mrefu.”

Niseme, “Naam, hiyo ni nzuri, naam. Hakika ni nzuri, pia, na kweli unaweza kuitumia.

“Naam.”

Niendelea, nizungumze naye kidogo. Niseme, “Ni... Je, umewahi kusikia juu ya nyundo *fulani-fulani* mpya?”

“La, siamini niliwahi kusikia.”

⁶¹ “Vema, hii *hapa*. Wewe weka misumari yako *hapa* ndani, na hebu tuzipigilie tu hizo mbao hapo chini. Angalia ule muda hii inaotumia, na ni bidhaa ya jinsi gani niliyo nayo!” Mwonyeshe hivyo. Useme, “Ichukue, ijaribu kwa siku chache uone unachowazia juu yake, nitarudi.” Unaona? Kama ni bidhaa nzuri, itajiuza yenyewe. Mnajua ninalomaanisha, sivyo, ndugu? Mnaona?

⁶² Mnaona, tuna Kitu kifaacho, hatuna budi kuwaendea watu Nacho vizuri. Mnaona? Jambo ndilo hilo, mnaona. Ni Kitu halisi cha kweli. Huyu ni Roho Mtakatifu, ninaamini kwa moyo wangu wote.

⁶³ Siamini ya kwamba ndugu ni wahaini, ninaamini wao ni ndugu. Siamini ya kwamba Roho afanyaye upambanuzi ni mpiga ramli yeyote, ninaamini ni Roho Mtakatifu akijifunua Mwenyewe katika Kanisa Lake, akilifanya tu Kanisa lipafikie mahali Pake.

⁶⁴ Na kama tungeweza tu kuwa na njia fulani ambayo tungeweza kuuchukua mwenendo wote wa Kipentekoste, na kubomoa tu vizuizi vyetu vidogo, na mahali pa kukutania, na kuketi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, ambapo tumebatizwa kwa Roho mmoja, loo, ninafikiri kungekuwako na madhihirisho ambayo hayajawahi kujulikana hapo kabla. Na kama tungeweza kuwaendea Wamethodisti, Wabaptisti, Wapentekoste, tungeweza kwenda kila mahali hata kila sehemu, ninaamini ingeweza kufanyika.

⁶⁵ Ndugu, sitaki kusimama hapa, ninataka kusoma Neno moja tu ama mawili kutoka katika Biblia na kuzungumza

nanyi kwa muda kidogo tu. Lakini nilitaka . . . Ninajua hamna budi kwenda, nami pia, nami ni—nina kile kiamshakinywa . . . Jumamosi asubuhi, na—na halafu tunatarajia kukaa Jumatatu usiku pia, mwingine huku chini. Sijui bado, sina budi kuzungumza na Ndugu Borders, na kadhalika. Lakini ninataka kuwaachia jambo hili, kwamba niko hapa kuwasaidia. Ni ninii tu . . . Hatuna ila kuketi tu pamoja dakika chache. Laiti tungaliweza kukaa hapa mpaka ibada itakapoanza alasiri ya leo, kisha asubuhi turudi tena, nami nisikilize yale mliyotaka kusema ninyi ndugu. Na jinsi ninavyolithamini!

⁶⁶ Lakini mimi, kuwajulisha tu moyo wangu, ninawathamini, nami nitafanya yote niwezayo kuwasaidia, kama ndugu zangu, kwa, kwa huduma ndogo ambayo Bwana amenipa, na yale aliyowapa ninyi, kwamba tunayaweka pamoja sasa, kuona kile tunachoweza kufanya kwa ajili ya Ufalme Wake.

⁶⁷ Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja tu, kabla hatujalikaribia Neno Lake.

⁶⁸ Mungu Mwenye Neema sana, katika Jina la Yesu Kristo, tunakuja Kwako na roho nyenyekevu, zilizovunjika, zenye toba, Bwana, tukijua ya kwamba tuko tayari kwa ajili ya kufinyangwa, kama vile nabii alivyoshuka kwenda kwenye nyumba ya mfinyanzi kufinyangwa. Na Baba, tunatamani, asubuhi ya leo, mioyoni mwetu, kwamba utatuvunja ili kwamba tutafinyangwa katika tabia mbalimbali, tabia ambazo zitamwakilisha Yesu Kristo.

⁶⁹ Chukua moyo wangu mjinga, Bwana, chukua maneno yangu yanayogugumiza na uyavunje vipande-vipande, Bwana, vunjilia mbali mapenzi yangu mwenyewe, na kufanya mtu mpya katika Kristo. Tujalie, Bwana. Hiyo ndiyo shauku ya mioyo yetu, hiyo ndiyo sababu tuko hapa.

⁷⁰ Pia, Bwana, tunapozungumza na Wewe juu ya madhabahu hii, ambapo maskini ndugu huyu wa Kiyahudi, anayekuamini Wewe, Ndugu Michaelson, ni—ninamwomba, Baba, ninaomba ya kwamba Wewe utambariki. Nasi tunashukuru kwa ajili ya fursa ya kuwa hapa katika sinagoga hili la Kikristo.

⁷¹ Tubariki pamoja sasa, tunapongojea tu kwa dakika chache kusomwa kwa Neno, libariki kwa mawazo yetu. Bariki ibada zetu, Bwana. Mungu, Wewe unaujua moyo wetu. Nami ninataka tu kuunganishwa kwa moyo mmoja, na nafsi moja, katika kusudi moja, hiyo ni pamoja na ndugu zangu hapa. Kwamba . . . Hapa katika nchi hii yenye giza, yenye huzuni, ya karne hii ya ishirini, hapa chini katika mwaka wa 1962, karibu na mwisho wa karne moja tena, wakati umewadia.

⁷² Na huku kwenye Pwani ya Magharibi, ambapo ustaarabu umesafiri kutoka mashariki hadi magharibi, nasi tunatambua ya kwamba hauwezi kuendelea mbele zaidi sasa, tunarudi mashariki tena tunapoondoka kwenye pwani hii, na kama vile

ustaarabu ulivyokuja, tunatambua jua husafiri mashariki hadi magharibi. Na kulikuwa na wakati ambapo yule M-w-a-n-a alikuja juu ya watu wa Mashariki, naye akaonyesha Nuru kuu, na ishara kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi.

⁷³ Naye aliahidi . . . Nabii alisema kutakuwa na siku ambayo isingeweza kuitwa mchana wala usiku. Tumekuwa na siku hii yenye huzuni, yenye ukungu ya karibu miaka elfu mbili, ya kuweza tu kuamini Nuru ya kutosha kutembea huku, na—na kujua ya kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu, na kujijengea kanisa, na shirika, na kujaribu kuwaweka ndugu na dada pamoja, na kuwaita waishi sawa, lakini, Bwana, ukungu unaondoka, Nuru inakuja juu ya watu wa magharibi, M-w-a-n-a yule yule akiwa na ishara zile zile, Injili ile ile, kurudishwa.

⁷⁴ Uliahidi katika siku za mwisho kwamba utakuja Ujumbe ambao ungeirudisha imani ya watoto iwarudie baba zao. Ee Mungu, jalia turudi kwenye Siku hiyo asilia ya Pentekoste, jalia turudi kwenye ile imani kuu waliyokabidhiwa watakatifu mara moja.

⁷⁵ Jalia ule Mti mkuu wa Bibi-arusi wa Mungu, ambao tunutu wameula wakaumaliza, uzae juu yake tunda ambalo Nuru za jioni zitaivisha kwa ajili ya kuja kwa Mwana wa Mungu. Tujalie, Bwana. Tusaidie tunapougana pamoja kwa kusudi hili.

⁷⁶ Tunajikabidhi Kwako, sisi ni Wako, fanya nasi, Bwana, upendavyo. Tunajikabidhi asubuhi ya leo katika sinagogi hili, mikononi Mwako, Bwana. Kusudi lako kuu na litimizwe maishani mwetu tunapojitolea kabisa Kwako, sio kama Samsoni, Samsoni alitoa nguvu zake, bali kamwe hakuutoa moyo wake. Mungu, jalia moyo wetu, nguvu zetu, yote yetu, yote yetu yatolewe Kwako, lifanye liwe na nguvu, Bwana, lizidishe kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

Katika Zaburi ya 16, kwa njia tu ya kusoma, kifungu cha mwisho:

Utanjulisha njia ya uzima: na mbele zako ziko furaha tele; katika mkono wako wa kuume kuna furaha ya milele.

Na sasa, mnajua nisingejaribu kuhubiri, ningependa tu kuzungumza nanyi kwa dakika moja, ama tuseme kwa mfano, kama dakika kumi na tano, ishirini.

⁷⁷ Daudi hapa alikuwa akinena juu ya uzima, “Wewe utanionyesha njia ya uzima.” Mliona jambo hilo? “Utanionyesha?” Ama, “Waweza kunionyesha? Natumaini Wewe utanionyesha.” “Wewe *utanionyesha*.”

⁷⁸ Ninaamini ya kwamba kila mtu ambaye Mungu amemwita atasikia na atakuja. Ninaamini ya kwamba hilo ndilo tunalolikabili sasa katika mkutano wetu. Tunaweza tu kupanda

Mbegu. Zingine zitaanguka kando ya njia, zingine zitaanguka upande mmoja, na zingine zitaanguka upande mwingine, lakini zingine zitaanguka kwenye udongo mzuri. Hiyo ni kweli. “Nionyeshe njia ya Uzima.”

⁷⁹ Sasa, uzima ndicho kitu kikuu sana ambacho tungeweza kupata. Hakuna kitu kilicho kikuu kuliko uzima. Kama ningeweza kwenda Utukufuni asubuhi ya leo, nasi sote tungeweza kwenda kule juu, nami ningeweza kukutana na Ibrahimu:

“Ni kitu gani kilicho kikuu kuliko vyote kilichopo Ibrahimu?”

⁸⁰ Angesema, “Uzima.” Hapo...Haidhuru kitu kingine chochote ni nini, uzima ndio kitu kikuu kuliko vyote ambacho mtu yeyote anaweza kupata, ni uzima. Ungetoa nini kwa ajili ya uzima?

⁸¹ Nina kitabu nyumbani, nacho kilikuwa, ninaamini, kiliandikwa na Ndugu Nugent, kasisi kutoka magerezani. Naye anatoa shuhuda katika kitabu hiki za watu mashuhuri waliokufa duniani, na, tangu wakati wa Kristo na kuendelea. Kisha anatoa ushuhuda wa watu mashuhuri waovu, na ushuhuda wa watu mashuhuri wa kiroho upande huo mwingine wa kitabu. Nami nilikuwa nikisoma pale, ninaamini ilikuwa ni Mary Aliyejaa Damu wa Uingereza, ambapo alisema, “Laiti ningeweza, loo, ningetoa ufalme wangu nipate kuishi dakika zingine tano!” Ufalme aliokuwa amewaua watu wengi sana kwa sababu, na kadhalika, na hata hivyo, angeutoa ufalme huo apate kuishi dakika tano zaidi.

⁸² Ningali ninakumbuka ushuhuda wa Paul Rader papa hapa nje, wakati alipokufa kule maskanini, ama, ambapo...alikuwa na ile maskani, aliposema...Alipokuwa akifa, alimwita Luke, ndugu yake, kwa namna fulani walikuwa marafiki kama mimi na Billy Paul, mwanangu,. Na kama vile nilivyosikia, kutoka kwenye—kwenye shule ya Moody, ambamo walikuwa na kundi la waimbaji wanne mle ndani, wakiimba, naye Paulo alikuwa na ucheshi, walikuwa wakiimba *Karibu Na Wewe Mungu Wangu*, naye akasema, “Aisee, kwani ni nani anayekufa hapa, mimi au ninyi?” Kisha kasema, “Fungueni hayo mapazia, mkaniimbie nyimbo tamu za Injili.” Nao wakaanza kuimba *Huko Chini Msalabani*, kitu kama hicho, kundi la waimbaji wanne.

⁸³ Naye akasema, “Yuko wapi Luke?” Alikuwa kwenye chumba cha pili, wakamleta. Akaushika mkono wa Luke, akasema, “Luke, liwazie, katika dakika tano kuanzia sasa, nitakuwa nimesimama katika Uwepo wa Yesu Kristo, nimevikwa haki Yake.” Naomba niende namna hiyo.

⁸⁴ Dwight Moody, mnajua kilichokuwa ushuhuda wake, wakati alipoinuka, alisema, “Ati haya ndiyo mauti?” Kasema, “Hii ni

siku yangu ya kuvikwa ukuu!” Hivyo ndivyo ninavyopenda kwenda.

⁸⁵ Niliushika mkono wa mama yangu wa thamani, hivi majuzi tu, akiondoka, niliushika mkono wa mke wangu wakati alipoenda, nimewaangalia wanapofikia mwisho wa safari, uzima ndio kitu kikuu kuliko vyote kilichopo. Na wale wasio na matumaini baada ya huu kwisha, ni jambo baya sana.

⁸⁶ Tunatembea kwenye mapito ya uzima. Watu wengi sana husema, “Uzima ni nini? Ninaweza kuupata wapi?” Mbona, umetuzunguka tu kote! Mungu ameufanya ninii sana . . .

⁸⁷ Kama vile katika Ayubu pia, tunaona katika ni—ninii . . . katika Ayubu, yeye aliuliza habari zake. Yote . . . kote maishani tunasikia, tukiuliza habari zake.

⁸⁸ Inanikumbusha juu ya m—mvulana mdogo aliyeishi huko chini Jeffersonville, ninakoishi. Siku moja, walisema alikuwa . . . alimwendea mama yake, naye akasema, “Mama, Mungu, Mungu huyu mnayenena habari zake, Yeye ni Mtu mkuu sana, kuna mtu angeweza kumwona?”

Akasema, “Mwulize mchungaji.”

⁸⁹ Kwa hiyo, akaenda kwa mchungaji na kumwuliza, akasema, ama, la, mwalimu wa shule ya Jumapili, naye mwalimu wa shule ya Jumapili akasema, “Afadhali umwulize mchungaji,” hakujuu.

⁹⁰ Kwa hiyo, akaenda kwa mchungaji, akasema, “La, la, mwanangu,” akasema, “hakuna mtu awezaye kumwona Mungu akaishi,” kasema, “humwoni Mungu.” Vema, kidogo lilimvunja moyo maskini jamaa huyo.

⁹¹ Basi kulikuwako na mzee mvuvi, naye alikuwa huko juu mtoni, siku moja, pamoja na maskini mvuvi huyu, akivua samaki, ndipo kukatokea dhoruba. Kama wengi wenu, nadhani, mmetoka mashariki na mnajua jinsi ninii . . . inavyofagilia mbali majani. Naye alikuwa akishuka mtoni, naye mvulana huyo mdogo alikuwa ameketi nyuma ya mtumbwi, nalo jua lilikuwa linatua magharibi, nao upinde wa mvua ukavuka mto namna hiyo, huku yule mvuvi mzee, akipiga makasia, maji yalikuwa yametulia kutokana na dhoruba, na kila kitu kilikuwa shwari, na harufu ya maua. Naye alipokuwa akipiga makasia, machozi makubwa ya fedha yakaanza kutiririka ndevuni mwake, alipotazama.

⁹² Maskini mvulana huyo akaangalia kote aone kile alichokuwa akiangalia, akamwangalia huyo mzee mvuvi, akakimbia kutoka kwenye hanamu ya mashua, hadi katikati ya mashua, naye akaketi karibu na magoti ya huyo mzee mvuvi, naye na kusema, “Bwana, nataka kukuuliza jambo fulani, mama yangu hawezi kunijibu, mwalimu wangu wa shule ya Jumapili, wala mchungaji wangu.” Kasema, “Je, . . . Mungu, kwa kuwa ni mkuu sana, je, mtu yeyote angeweza kumwona?”

93 Ndipo huyo mzee mvuvi akavuta makasia pajani mwake, akaweka kichwa cha mvulana huyo mdogo begani mwake, kasema, “Mungu aubariki maskini moyo wako, kipenzi. Yote ambayo nimeona kwa miaka arobaini iliyopita yamekuwa ni Mungu.” Mnaona? Yeye alikuwa tu . . . Inakubidi kuwa na Mungu *hapa* ndani ili kumwona *huko* nje, unaona. Mungu aliye *ndani* akiangalia kupitia macho yako.

94 Ninaangalia upande wa pili wa barabara kwenye mti. Ninawazia sasa, nilipopitia kwenye jangwa la Mojave, ama, jangwani nikija huku chini, kila kitu kilionekana kimekufa sana, na mara tu nilipofika kule karibu na Mto Colorado, kulikuwako na kichaka kimoja kidogo cha kijani kibichi, kilionekana wazi sana. Nikawaza, “Ni wapi ninii wake . . . kinatoa uhai wake wapi?” Mnaona, kilikuwa na uhai, kilikuwa hai. Mungu yuko katika—katika uhai. Yeye ni . . . Kila kitu kilicho hai kina Mungu ndani yake.

95 Ayubu alisema siku moja, “Mti ukifa, utaishi tena. Lakini mwanadamu hulala chini, hutoa roho, yeye . . . naye yuko wapi? Wanawe wanakuja kuomboleza na kumpa heshima, lakini yeye hajui. Ee, laiti ungenificha kaburini, na kuniweka mahali pa siri, hata ghadhabu Yako itakapopita!”

96 Naye a—aliona, alimwona Mungu katika maumbile Yake, uhai, jinsi ua dogo linavyochipuka, linasimama hapo, baada ya kitambo kidogo linapendeza, na kuna machipukizi kwenye tuta la—la maua, na mengine yenye umri wa makamu, na mengine yenye umri mkubwa, lakini jalidi inapokuja na kuyapiga, inayaua yote. Nalo ua dogo linaangusha maskini petali zake, na kutoka kwenye tumba hilo la ua, kuna mbegu ndogo nyeusi, jamaa mdogo, mdogo sana, anaanguka. Na kadiri linavyoonekana la ajabu, lakini hata hivyo, Mungu ana msafara wa mazishi kwa ajili ya ua hilo. Mlijua hivyo? Mvua ya masika inakuja, na Yeye analia machozi makubwa ya maji, na kuzika hiyo mbegu ndogo ardhini. Moja kwa moja inakuja baridi kali ya kipupwe, na kuligandisha, inapasuka, utovu unatoka ndani yake.

97 Kila kitu cha kimaumbile ambacho ungeweza kuangalia kimetoweka. Mwanasayansi angeweza kuchukua konzi ya uchafu huo, na kuupeleka kwenye maabara, na kuichunguza kwa makini, wala huwezi kupata chembe hiyo ya uhai, haipo. Po—potashi, na kalisi, na petroli, na unyevu, kila kitu kilicho ndani yake kimerudi mavumbini, lakini mahali fulani mle ndani pamefichwa chembe ya uhai, na kwa hakika tu kama vile jua linavyochomoza tena katika majira ya kuchipua, litaishi tena, Mungu ameliandalia njia.

98 Hebu chukua na kuweka zege uani mwako kwenye majira ya baridi kali, weka mawe. Je, tumba lako kubwa zaidi la nyasi liko wapi? Liko moja kwa moja ukingoni mwa unjia wako. Kwa nini?

Ni mbegu hizo zilizokuwa zimefunikwa, ndipo wakati jua hilo linapoanza kuangaza juu ya uhai huo wa mimea, maskini mbegu hiyo ya uhai itapenya zege hiyo yote, juu ya kila mwamba, chini ya kila kijiti, na kujongea karibu mpaka inachomoza maskini kichwa chake nje, na kumsifu Mungu wa uzima. Kamwe huwezi kuuficha uhai. Hiyo ndiyo sababu ya sisi kuwa hapa, ndugu, kuleta Uzima.

⁹⁹ Si muda mrefu uliopita nilikuwa nimeketi, nikila chakula cha jioni pamoja na maskini mhudumu Mmethodisti, mzee mtakatifu mwenye neema wa Mungu, alikuwa na Roho Mtakatifu maishani mwake. Nasi tulikuwa tukisikiliza, *Majira ya Kilimo* kikaja kutoka Louisville, nacho kilabu cha 4-H kilikuwa na mtambo ambao wangeweza kutengeneza punje moja ya mahindi kikamilifu sana, hata ingepika ugali mzuri sana wa mahindi kama wa yale yaliyokuzwa kutoka shambani, chembe za mahindi aina ile ile. Na kwa kweli, ungeweza kuzikatakata, uziweke kwenye maabara, na ninii...moyo wake ulikuwa mahali panapofaa, kiasi kinachofaa cha unyevu, na potashi, na yote yaliyo kwenye mahindi. Usingeweza kuyatofautisha, ukiisha kuyachanganya pamoja, usingeweza kuyatofautisha moja kwa lingine, yalikuwa makamilifu sana.

¹⁰⁰ Akasema, “Njia pekee unayoweza kujua ipi ni ipi ni kuyazika.” Yale yaliyotengenezwa na mtambo yataoza, na ni hayo tu, bali yale ambayo Mungu aliyakuza, yana uhai mle ndani ambao utafufuka tena.

¹⁰¹ Mtu anaweza kuonekana kama Mkristo, aigize Mkristo, ama atembe kama Mkristo, ama kadhalika, bali isipokuwa chembe hiyo ya Uzima iwepo, hawezi kufufuka tena.

¹⁰² Yesu alisema, “Nilikuja wapate kuwa na Uzima,” Zoe, Uzima wa Mungu Mwenyewe ndani yao. Na kuna...Kila kitu kilichokuwa na mwanzo kina mwisho. Ni vile vitu ambavyo havikuwa na mwanzo ndivyo havina mwisho, kuna Kitu kimoja tu ambacho hakikuwa na mwanzo, hicho kilikuwa ni Mungu. Nasi tunakuwa watoto Wake, sehemu Yake, halafu Zoe, Uzima wa Mungu Mwenyewe, Uzima wa Milele, tumepewa sisi, na hiyo ndiyo njia pekee tunayoweza kuishi. Na hiyo ndiyo njia pekee ambayo marafiki zetu waliopotea huku nje, hata washiriki wa kanisa, wanaweza kuishi tena, ni kwa sababu wamepewa Zoe, nasi tunakuwa sehemu yake.

¹⁰³ Je, mliona kwenye Siku ya Pentekoste? Jinsi ambavyo Nguzo hii kuu ya Moto (Ambayo sote tunajua ilikuwa ni Mjumbe wa lile agano, ambaye alikuwa ni Yesu Kristo, ambapo Musa alihesabu kushutumiwa kwa Kristo kuwa ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri, kwa kuwa aliiacha Misri, akimfuata Mjumbe yule mkuu, Nuru hii.), kwenye siku ya Pentekoste, wakati Nuru hii kuu ilipoingia mle, Mungu alijigawa Mwenyewe! Ndimi za Moto zikamkalia kila mmoja wao, nao wote wakajazwa na Roho

Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha zingine, kama Roho alivyowajalia kunena, Mungu akijigawa Mwenyewe kutoka kwenye Mwenye uhai mmoja hata akawa Kanisani Mwake, akiugawa Uzima Wake pamoja na watu Wake. Huo ndio Ujumbe tunaopaswa kuwafikishia watu, wataangamia bila Huo, hawana budi kuangamia.

¹⁰⁴ Mama yangu mwenyewe ameaga dunia hivi majuzi. Niliposimama karibu naye, naye akasema, “Billy,” watoto wetu wote walikuwa, uh, watoto wake walikuwa wamesimama pale, waliokuwa hai, wawili wetu walikuwa wameaga kati ya kumi. Ndipo huyo msichana . . . akaniangalia, naye akasema . . . kwanza akamwangelia Delores, akasema, “Wangu wa mwisho, na wangu wa kwanza.” Naye mama alikuwa Mkristo mwenye neema, nami nilikuwa nimemwongoza kwa Kristo na kumbatiza miaka mingi iliyopita.

¹⁰⁵ Naye akasema, “Delores, umekuwa mwema kwangu, umenisaidia. Ume—umenifulia mara nyingi wakati nimezeeka wala siwezi kufua. Umeshuka ukaja kuisafisha nyumba yangu, ungefanya mambo haya.” Akasema, “Nakupenda, Mpenzi.”

Naye Delores, Mkristo mchanga, amesimama pale akihema, akiangalia chini, naye akasema, “Mama, yalikuwa madogo sana.”

Akasema, “Billy, ulihakikisha ya kwamba sikushinda njaa.”

¹⁰⁶ Ndipo nikasema, “Mama, ni mara ngapi umeondoka mezani ili nipate chakula, wakati tulipokuwa . . . hatukuwa na chakula?” Nami nikasema, “Ilikuwa tu ni wajibu, Mama.”

Naye akasema, “Basi kwa namna fulani umekuwa kiongozi wa kiroho kwangu, Billy. Ulinibatiza, umeniambia njia ya Uzima.”

¹⁰⁷ Nikasema, “Mama, unajua asili yetu ni Katoliki,” nami nikasema, “nami ni—ni—nilienda kanisani, lakini wao wakasema, ‘*Hili* ndilo kanisa,’ nalo lilikuwa ni kinyume na Neno. Nilienda kutoka kanisa moja hadi lingine, nami nikakuta kwamba lilikuwa kinyume sana, kwa hiyo nikadumu na Neno, Mama.” Nami nikasema, “Nimejaribu kukwambia yaliyo kweli na kukuongoza kwa Kristo.” Ndipo maskini huyo mtakatifu mpendwa akaenda kukutana na Mungu, kisha nikaikabidhi nafsi yake kwa Mungu.

Delores akanipigia simu, naye akasema, “Billy, si—siwezi kulivumilia,” akasema, “Mama.”

Nikasema, “Delores, hebu angalia upande wa pili wa barabara kutoka mahali unapoishi. Hivi hakuna mwaloni mkubwa uliosimama hapo?”

Akasema, “Naam.” Hii ilikuwa ni siku chache tu kabla Mama hajafariki. Naye akasema, “Naam.”

Nikasema, “Majira ya kupukutika yanakuja sasa.”
Nikasema, “Yapata mwezi mmoja uliopita majani hayo yalikuwa mazuri sana na ya kijani kibichi.”

“Naam,” akasema, “Bill.”

Nikasema, “Ni lini . . . ? Yanaonekanaje sasa?”

Naye akasema, “Vema, ni manjano, na kahawia, na kijani kibichi, mekundu.”

Nami nikasema, “Delores, ni kitu gani kinachoyafanya yawe manjano, kahawia, kijani kibichi, na mekundu?”

Akasema, “Yanakufa.”

Nikasema, “Je, ni lini huo mti ulikuwa wa kupendeza zaidi?”

Akasema, “Sasa.”

¹⁰⁸ Nikasema, “Biblia ilisema, ‘Ina thamani machoni pa Bwana mauti ya watakatifu Wake.’” Mnaona? Hapo ndipo wakati unapofika. Nikasema, “Ule uhai unarudi tena. Uhai ni mti, sote tunaning’inia kwenye ule Mti wa Uzima.” Hiyo ni kweli.

¹⁰⁹ Bw. Wood, ambaye ni mwuza vitabu mkutanoni, yeye alikuwa ni Shahidi wa Yehova. Naye alikuwa . . . alikuwa na mvulana, ambaye yuko pamoja naye pia, mguu wake ulikunjamana namna *hii* kwa polio. Naye alikuwa huko Louisville katika mmojawapo wa ile mikutano, naye akaona upambanuzi huo, ndipo akasema, “Sasa, hilo linaonekana sawa kwangu.”

¹¹⁰ Na kwa hiyo akaenda Houston, Texas, nilipokuwa kule pamoja na Ndugu Kidson na hao wengine, wakati ile picha ya Malaika wa Bwana ilipopigwa. Na, vema, imepigwa mara kadhaa, na hivi majuzi tu, ni, ya—yake kupigwa tena, ilipigiwa huko Ujerumani, na mara nyingi.

¹¹¹ Kwa hiyo, na—naye Ndugu Wood alikuwa amemleta mvulana wake, naye alikuwa huko kwenye mmoja wa hiyo mikutano, nao walikuwa wameketi huko nyuma kabisa, loo, karibu nusu jengo la mji, ama mbali zaidi. Usiku mmoja, nikisimama jukwaani, sikuwahi kusikia habari zake maishani mwangu, nikisimama tu pale nikiangalia huku na huku, nikaona ono mbele yangu, nami nikasema, “Kuna mtu, ameketi huko nyuma kabisa, yeye na mke wake, nao wanatoka jimbo la Kentucky, huko chini kabisa mahali panapoitwa LaGrange, Kentucky. Jina lake ni Wood, yeye ni seremala, ana mvulana aliye na madhara ya polio ambayo yameuvuta mguu wake juu. ‘BWANA ASEMA HIVI, huyo mvulana ameponywa,’” ndipo akaanza tu namna hiyo. Naye mke wake alikuwa Mmethodisti, kwa hiyo, ama, ninaamini Church of God, Kanisa la Church of God la Anderson.

¹¹² Kwa hiyo, kasema, “Ulisikia hilo, Ruby?” Na kwa hiyo, akasema, “David, simama.” Mguu wake ulikuwa mkamilifu

tu kama huo mwingine. Yuko humu mkutanoni. Ndipo huyo Shahidi wa Yehova akajisalimisha kwa Kristo.

¹¹³ Halafu basi, kutoka hapo akashuka ndugu yake. . . Loo, wao, mnajua jinsi wao, Shahidi wa Yehova wanavyojisikia. Walishuka wakaja kumwondosha ndugu yake kwenye. . . kutoka kwenye ushirika wao. Akasema, “Ati unasikiliza kitu kama hicho,” kasema, “mambo haya ya uongo yanayoenezwa namna hiyo? Umekuwa. . .” Baba yake ni msomaji katika Mashahidi wa Yehova. Akasema, “Unajua vema kuliko kitu kama hicho.” Akasema, “Kama nikipata kumwona mtu huyo, nitamwambia ukweli wa mambo.” Kasema, “Najua, mafundisho aliyonipa baba yangu.”

Kasema, “Ndiye yule anayekata nyasi pale nje.”

¹¹⁴ Nami nikaingia na kofia chakavu iliyoinama, mwajua, nikaketi chini, nikazungumza naye. Akasema, “Vema,” akasema, “nitakwambia, Bw. Branham,” akasema, “tulilelewa Mashahidi wa Yehova.”

¹¹⁵ Nikasema, “Hilo ni sawa kabisa.” Nikasema, “Afadhali niwe *Nuru-ruseli* kuliko kutokuwa Nuru hata kidogo,” naye akaendelea tu namna hiyo, bila kupuuza lolote alilokuwa a—amesema, na kuzungumza naye vizuri nilivyoweza. Nami nikasema, “Ninaona kwamba wewe ni mtu aliyepoa, nawe una watoto wawili.” Naye. . . Nikasema, “Lakini umeachana na mke wako.”

¹¹⁶ Ndipo akamwangukia Banks. Huyu ni Bw. David, baba ya David Wood, yule aliye hapa mkutanoni. Akaangukia huko, akafikiri labda Bw. Wood alikuwa ameniambia hayo, nami nikashika wazo lake upesi sana, mnaona.

¹¹⁷ Kwa hiyo nikasema, “Ulidhani Ndugu Banks alikuwa ameniambia hilo, hakuniambia, hajaniambia lolote kuhusu familia yake.” Lakini nikasema, “Labda unafikiri kama Banks aliniambia hivi: Hivi majuzi usiku ulikuwa na mwanamke mwe—mwenye nywele za hudhurungi. Ulikuwa chumbani pamoja naye wakati mpenzi wake alipokuja mlangoni, na kubisha mlangoni, naye akaenda mlangoni, wala asingekuruhusu uje, nawe ukaangukia dirishani. Lilikuwa ni jambo zuri, angeupiga risasi ubongo wako.” Nikasema, “Huyo mtu akiwa amesimama pale amevaa suti nyeusi, tai nyekundu.”

¹¹⁸ Loo, karibu aanguke sakafuni! “Hiyo,” akasema, “hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli.” Na hapo nikambatiza siku chache baadaye, huyu hapa baba yake anashuka. Huyu hapa dada ya—yake anashuka, alikuwa ashuke aje, awanyoshe hao wavulana wote wawili. Nikambatiza siku ile ile alipokuja, kwa jambo lile lile. Akashuka baba yake, naye alikuwa akitaka kutunyoosha sote. Kwa hiyo alitaka kutupeleka. . .

¹¹⁹ Nikasema. . . Yeye alikuwa ni mvuvi, nikasema, “Sasa, Banks, hebu tumpeleke akavue samaki.” Kwa hiyo tukaanza

kuvuka mto. Ilinyesha usiku kucha, mnajua jinsi ilivyo huko mashariki, hiyo mito hufurika, na kadhalika. Tulikuwa tukishuka kwenda kwenye Bwawa la Wolf Creek. Na barabarani huko. . . Hakusema lolote kuhusu dini bado, mzee mkali sana. Naye akasema. . . Na mwerevu awezavyo kuwa. Kwa hiyo tukavuka mto.

¹²⁰ Nikasema, “Vema. . .” Nikaona ono likija mbele yangu pale nilipokuwa nimeketi, Banks alikuwa akiendesha gari, nikaliangalia lile ono. Nikasema, “Sasa, kila kijito tutakachovuka. . .”

Alikuwa tu amesema, usiku huo alisema, “Kama ningeweza kuona jambo kama hilo likitukia, ningeamini.”

¹²¹ Na kwa hiyo asubuhi hiyo, neema ya Bwana, nikasema, “Tunaninii. . . Kila kijito tutakachovuka kitakuwa kimejaa matope. Tutakapofika kwenye Bwawa la Wolf Creek, mvua ilipanda juu ya bwawa na hapo, ama, chini ya bwawa, hasa, wala hakutakuwa na matope, nasi tutavua samaki leo, hatutashika chochote leo mpaka jioni. Halafu Bw. Wood hapa, Banks Wood, utamshika kambare mmoja mdogo, nitashika kama ratili ishirini, na baadhi yao watakuwa na uzito wa ratili kumi kila mmoja. Mtavua samaki kwa chambo ile ile mahali pale pale, hamtashika chochote. Tutavua hadi yapata saa tano usiku, samaki wataacha kuuma. Tutaingia na kula—na kula chakula chetu cha jioni saa tano usiku, tukae usiku kucha. Ndipo kesho yake asubuhi, tutatoka, nami nitamshika samaki mkubwa aliye na magamba, na hicho kitakuwa ndicho kitu cha mwisho kitakachoshikwa. Hatutaninii. . . tutavua siku nzima, tusipate kitu.”

¹²² Ndipo huyo mzee akaangalia kote, kidogo namna *hiyo*. Tukashuka, na kila kitu kilitukia kikamilifu kabisa, jinsi kilivyotukia. Ndipo nilipofika kwenye zile mbao jioni hiyo, yeye akasema, “Haya hapa maji; ni kitu gani kinachonizuia nisibatizwe?” Basi hilo hapo kundi zima lao. Loo, ni jambo tukufu kujua ya kwamba tunaning’inia kwenye Mti!

¹²³ Sasa, kulikuwa na. . . Mimi na Bw. Wood tulikuwa tukiwinda kuchakulo. Kama mjuavyo, mimi. . . napenda kuwinda. Na kwa hiyo tulikuwa tukiwinda kuchakulo pamoja huko chini Kentucky, yapata miaka miwili iliyopita sasa. Nilikuja kwenye likizo yangu msimu huo wa kupukutika. Nami nimewinda Afrika, India, na karibu kote ulimwenguni, lakini mimi. . . alinipa tu asubuhi yenye ukungu Agosti, ama wakati mwingine huko juu. . . kwa bunduki ya .22. Na kwa hiyo basi, ninapenda tu kuwinda kuchakulo.

¹²⁴ Nasi tulikuwa huko chini Kentucky tukikaa majuma mawili, ndipo kukawa na joto sana. Sasa, wewe—wewe Mkalifornia huenda usijue ninalozungumzia, wakati majani na kila kitu

ni joto sana, na ninii...nawe unakanyaga hapo, ndipo hao kuchakulo wadogo wa kijivu... .

125 Nasi hulenga tu jicho, kwenye yadi hamsini. Kama yuko umbali wa yadi arobaini, tunarudi nyuma kwenye yadi hamsini, na kupiga risasi kwenye jicho. Wasiponinii... .kama ikipiga chini ya jicho lake, ama juu ya jicho lake, nenda ukabadilishe bunduki hiyo, kuna kasoro. Na kwa hiyo tunadumu moja kwa moja nayo, hivyo ndivyo ilivyo. Nimejaribu kujizoeza hilo, kulenga risasi mahali hapo hasa.

126 Na kwa hiyo, basi, huko juu kabisa tukipiga kambi, ndipo ikawa joto sana. Nao hao kuchakulo wadogo wa kijivu, mnanena juu ya Houdini kwamba ni bingwa wa kutoroka, yeye ni mwanagenzi kwa mmoja wa hao. Kugusa tu kichaka kidogo, naye huyo ametoroka.

127 Nyote mnamjua Ndugu G. H. Brown. Mwaluzeni tu juu yake wakati mmoja, tuliwinda pamoja. Kwa hiyo basi... .Nami ninamtania kuhusu maskini ile bunduki ya marisau inayojiendesha aliyonunuliwa na mke wake, mwajua, yapata miaka ishirini iliyopita, kwa hiyo, akiwapiga risasi kuchakulo kwa bunduki ya marisau.

128 Kwa hiyo basi, tulikuwa tukiwinda, na kulikuwa na... .Ndugu Wood akasema, “Unajua, Ndugu Branham,” akasema, “hapa mahali *fulani* kuna mabonde.” Sidhani mnayo huku California. Yako huko chini, chini, chini kabisa ambapo vijito humpitia na kuyatia unyevu. Wewe, huko juu kwenye ardhi tambarare, ukikigusa kichaka hicho, wametoroka. Huwezi kuwafikia, kwa kuwa... .Wanaenda umbali wa yadi mia mbili ama mia tatu. Wametoweka upesi *hivyo*. [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.]

Kwa hiyo basi, tulisema, “Tutaenda huku, tuone kama ataturuhusu kuwinda,” kasema, “ana yapata ekari mia tano.”

Nami nikasema, “Vema, hilo litakuwa sawa.”

129 Kwa hiyo tukashuka, si barabara nzuri kama mlizo nazo hapa, bali kupitia vijia vya nguruwe, na chochote kile, kupitia vichani, kuvuka mabonde, mpaka tukaingia mle. Akasema, “Sasa, kuna dosari moja tu kuhusu hili.” Kasema, “Mzee huyu,” kasema, “yeye ni kafiri, na, loo, yeye ni mkali.”

130 Nikasema, “Loo, ni—nitakuacha tu uzungumze.” Mnaona? Kwa hiyo nikaketi kwenye lile lori dogo, nasi tukaelekea kwenye nyumba nyeupe, nzuri nyeupe, huko nyuma kabisa chini ya kilima kikubwa, na—na shamba kubwa la magugu na shamba la mahindi upande *huu*. Tukaendesha gari, kulikuwako na wazee wawili wameketi huko nje, *Kentucky* kwelikweli. Nayo Kentucky ina njia yake ya kuishi, mwajua.

131 Ndugu David, kule nyuma, yule—yule ndugu Myunani, alisema, “Ndugu Branham, nilisikiliza kanda zako.” Kasema,

“Mimi . . .” Hivi kwa namna fulani ni vibaya sana kusema hili baada ya kiamshakinywa. Akasema, “Ulitaja ‘unywele katika biskuti.’” Kasema, “Nimelichunguza, siwezi kupata hiyo ni nini.”

¹³² Nami nikasema, “Hiyo ni Kentucky tu,” mnaona, “‘unywele katika biskuti.’” Nikasema, “Usijaribu kulitafuta hilo katika kamusi maana halitakuwepo.” Nikasema, “Huko Kentucky . . .”

¹³³ Kwa hiyo tukarudi kule nyuma kwenye bonde hilo la miti midogo, mwajua, na zile kofia kubwa za kale zikining’inia chini. Tukasimama, naye Ndugu Wood akatoka, akazunguka, kulikuwako na wazee wawili wameketi pale, naye akamwendea mmoja wao, akamwita, akasema, “U hali gani?”

¹³⁴ Naye akasema, “Njema, Bwana?” Naye akasema, “Mimi ni . . . Jina langu ni Wood, mimi ni Banks Wood.” Akasema, “Nashangaa . . . Tumekuwa tukiwinda hapa Dutton . . .” Nao huzipa sehemu zao majina ya vijito. Kasema, “Tumekuwa tukiwinda huko Dutton, nasi tukashangaa kama tungeweza kuwinda sehemu yako.”

Akasema, “Wewe ni Wood yupi?”

Akasema, “Mimi ni mvulana wa Jim Wood.”

¹³⁵ Akasema, “Chochote chao . . .” Hilo lilikuwa ni kundi moja la Mashahidi wa Yehova lililokuwa ni watu waaminifu. Akasema, “Chochote ambacho Jim Wood, yeyote wa watu wake, amekaribishwa kwa chochote nilicho nacho mahali hapa.” Akasema, “Mzee Jim, angali hai?”

Akasema, “Naam. Yeye yuko huko Indiana sasa,” kisha kusema, “Ninaishi huko nje pia,” akasema, “nami hushuka huku kuwinda kuchakulo kila msimu wa kupukutika.”

Akasema, “Karibu, nina ekari mia tano, na mabonde mengi na kadhalika. Karibu tu.”

Akasema, “Vema, asante, sana.” Akasema, “Nilikuja na mchungaji wangu.” Akasema, “Hungejali yeye akiwinda, pia?”

Akasema, “Wood, unataka kuniambia umekuwa duni sana hata inakulazimu kubebana na mhubiri popote uendapo?” Naye akasema . . .

Kwa hiyo nikawazia wakati umewadia, mimi nitoke kwenye gari. Kwa hiyo nikatoka kwenye gari, mwajua, na kwenda pale, nami nikasema, “Mu hali gani?”

Akasema, “Njema.” Kisha akasema . . . Kabla hawajanitambulisha, akaingilia moja kwa moja, akasema, “Vema,” akasema, “Sina haja sana na ninyi jamani.”

Nikasema, “Vema, ninapendezwa na uaminifu wako.”

¹³⁶ Na—naye akasema, “Sababu yake, ni jambo hili moja,” akasema, “kwanza kabisa, huonekani kama mhubiri.” Damu ya kuchakulo na masharubu, wala sikuwa nimeoga kwa majuma

mawili. Mimi . . . Hmm! Kwa hiyo nikasema, “Vema, na—nadhani hiyo ni kweli, pia.”

Naye akasema, “Jambo nililo nalo dhidi yenu enyi jamaa, mnabwekea mti usio na kitu ndani yake.”

¹³⁷ Sasa, sijui kama mnajua hiyo ni nini. Hilo ni lingine la *Kentucky*, David, usijaribu kutafuta hilo katika kamusi. Wakati mbwa mwinda rakuuni ni mwongo, atakimbilia mti fulani, naye kuuni yuna ujanja, atakimbia, aruke juu ya mti, kisha aruke atoke huko, mnaona, na kama mbwa hajafunzwa vizuri, atakimbilia mti huu ambapo alimwona kuuni, akanusa mahali alipomfuatilia kwenye mti, na kusimama hapo na kubweka, wala hakuna kitu kwenye mti huo. Kwa hiyo kwa kawaida wanampiga risasi mbwa huyo.

¹³⁸ Kwa hiyo—kwa hiyo akasema, “Enyi watu, hicho ndicho mnachohitaji, risasi nzuri ya mbwa mwindaji,” akasema, “kwa sababu mnabwekea kwenye mti usio na kitu mle.” Mnajua ninalomaanisha, kuhubiri. Akasema, “Ninahesabiwa kuwa kafiri.”

Nikasema, “Vema, kila mtu kwa maoni yake mwenyewe, lakini kwangu mimi, hilo si jambo la kujivunia.”

¹³⁹ Naye akasema, “Vema,” kasema, “vema,” akasema, “jambo lenyewe ni kwamba,” kasema, “mna—mnazungumzia kitu fulani pale . . . ambapo hapana Kitu kama hicho.”

Kasema, “Naam, bwana.” Nikasema, “Bila shaka, hayo ni maoni.”

¹⁴⁰ Naye akasema, “Vema,” akasema, “ninyi jamaa mnaozungumza juu ya Mungu, wala hakuna Kitu kama hicho.” Naye akasema, “Kama kulikuwako na Mmoja ningeweza kumwona.” Kisha kasema, “Nimeishi miaka hii yote, nina umri wa miaka *sabini na kitu*,” kisha kasema, “Bado sijaona chochote Chake.” Naye akasema, “Hakuna Kitu kama hicho, nanyi watu mnabwekea mti mwingine, pia mnachukua pesa za watu kwa ajili ya riziki zenu, na mambo kama hayo, nanyi si kitu ila kundi la walaghai.”

¹⁴¹ Nikawaza, “Loo, jamani!” Nikasema, “Naam, Bwana, bila shaka hayo ni maoni.” Nikawaza, “Ee Mungu, usiponisaidia!” Kwa hiyo nikasema, “Naam, Bwana, hayo bila shaka, ni maoni,” nikasema.

¹⁴² Nanyi mwajua, Mama, maskini mama yangu wa kusini, daima alinipa ushauri mzuri, naye alinipa, alitoa tamshi wakati mmoja, akasema, “Mpe ng’ombe kamba ya kutosha, naye atajinyonga,” mnaona. Kwa hiyo nikafikiri hilo linamfaa, nimwache tu aendelee na kubweka kidogo, nasi tutaona amepanda mti gani, mnaona. Kwa hiyo basi, nikamwacha aendelee na kuzungumza, ndipo nikapata kitu fulani, kisha jambo fulani likaja niani mwangu.

143 Basi kulikuwako na mtofaa pale waliokuwa wameketi chini yake. Na kwenye msimu wa kupukutika mwakani hayo matofaa, ilikuwa yapata—yapata juma la mwisho la Agosti, ma—matofaa yalikuwa yakianguka, nao manyigu walikuwa wakiyala. Mnajua manyigu ni nini? Vema. Vema, kwani mnatoka sehemu gani ya Kentucky? Mnaona? Na kwa hiyo basi nikamwambia, nikasema, “Unajali kama nikichukua moja ya hayo matofaa?”

Akasema, “Karibu, manyigu wanayala.”

Nikanyoosha mkono nikaliokota, na kulisugulia kwenye suruali iliyojaa damu, mwajua, kisha nikalingw’afua, nikasema, “Jamani, ni tofaa zuri!”

Kasema, “Naam, ni zuri sana.”

Nikasema, “Inaonekana kana kwamba huzaa kwa wingi sana.”

“Naam, Bwana,” kasema, “Mimi huchuma pishi *kadhaa* kila mwaka kutoka kwake.”

“Huu mti una umri gani?” Kumbadilishia hoja, mwajua.

144 Naye akasema, “Loo,” akasema, “je, unaona mahali lile dohani la kale linaposimama pale?” Kasema, “Nilizaliwa huko juu.” Kasema, “Mama na Baba waliishi huko,” kisha kasema, “ndipo moto ukaiteketeza. Tukajenga nyumba hii mpya hapa chini.” Kisha kasema, “Basi nikalelewa hapa juu.” Kisha kasema, “Baba na Mama walipokufa, ni—nilikaa tu na hii nyumba.” Kisha kasema, “Basi tulipohamia hapa chini, niliupanda mti huo hapo ndani miaka arobaini, hamsini iliyopita, ama kitu kama hicho.” Kisha kasema, “Umekuwa hapo tangu wakati huo.”

Nikasema, “Hilo ni jema.” Nikasema, “Jamani, hilo ni jema sana!”

Akasema, “Naam, Bwana.” Akasema, “Tukirudia kuwa mhubiri,” akasema, “Ninataka kukuuliza jambo fulani.”

Nikasema, “Naam, Bwana. Ni lipi?”

Akasema, “Enyi watu, kama mngeweza kutoa chochote, mbona, ingekuwa ni tofauti.” Akasema, “Sasa, nilimsikia mhubiri mmoja wakati mmoja, ama, nilisikia habari zake.”

145 Kasema, “Maskini Dada *Fulani* hapa juu kilimani,” kasema, “alikuwa akifa kwa kansa.” Kisha kasema, “Kulikuwa na mhubiri aliyekuja hapa Acton, Kentucky,” (Kweli, ilikuwa yapata maili thelathini kutoka hapo. Nami... Wood akaniangalia, nami ni—nikatikisa kichwa changu.), akasema, “huko kwenye uwanja wa kambi ya Methodisti.” Akasema, “Mhubiri huyu alitoka huko *Indiana*’r.” Naye akasema, “Akaja kule,” na kusema, “walisema kulikuwa na yapata watu elfu mbili mia tano waliokusanyika huko nje usiku huo.” Na hiyo

ni huko nyuma kabisa vilimani, mwajua, walikuja kwa mgongo wa farasi na kila kitu kufika huko.

¹⁴⁶ Kisha kasema, “Alikuwa huko siku tatu usiku.” Kisha kasema, “Kwenye usiku wa pili,” kasema, “dada ya maskini mama huyu mkongwe anaishi mahali paitwapo Campbellsville, basi wakati mhubiri huyu alipokuwa akihubiri, aliangalia nyuma katika kusanyiko, huko nyuma kabisa mahali mwanamke huyu alipokuwa na kuliita jina lake, na kusema, ‘Usiku wa leo, kabla hujaondoka nyumbani, uliangalia kwenye kabati la jikoni upande wa kushoto, ukachukua lesa ndogo yenye mchoro wa samawati pembeni mwake, unayo kwenye pochi yako, nawe una dada jina lake *Nanii*, ambaye anakufa kwa kansa ya tumbo. Nenda ukachukue lesa hiyo, ukaiweke juu ya huyo mwanamke, naye atapona.’”

¹⁴⁷ “Vema,” kasema, “karibu usiku wa manane usiku huo, tulidhani walikuwa na Jeshi la Wokovu kule juu ya kilima.” Akasema, “Sijawahi kusikia mngurumo kama huo maishani mwangu, nao walikuwa wakipiga mayowe.” Na kama yeyote wenu anajua, huyu alikuwa ni Ndugu Ben na hao wengine, huko juu wakiweka lesa hiyo juu ya huyo mwanamke. Kisha kasema, “Tulidhani labda maskini huyo bikizee alikufa. Basi kesho yake asubuhi,” kasema, “tulipanda kwenda kule kuona watakapofanya maandalizi kwa ajili ya mazishi,” tena kasema, “alikuwa ameketi pale mezani, yeye na mumewe, wakila sambusa za matofaa yaliyokaangwa na kunywa kahawa.”

¹⁴⁸ Mnajua sambusa ya matofaa yaliyokaangwa ni nini, nusu mwezi uliopinduliwa? Nina hakika niko nyumbani. Kwa hiyo wao. . .Mwajua, na—naipenda hiyo kama imepakwa sukari ya rojorojo. Mnaona? Wala sipendi kunyunyizia, na—nabatiza, mwajua, na kweli ninazimwagilia. Ninapenda sukari ya rojorojo nyingi kwenye sambusa yangu. Kwa hiyo ni—ninapenda sana vitu hivyo.

¹⁴⁹ Na kwa hiyo basi, alikuwa akila sambusa hii ya tofaa lililokaangwa. Kisha kasema, “Siku moja kabla ya hapo, alikuwa katika hali mbaya sana, hata tusingeweza. . .” Wasingeweza tena kumweka kwenye maliwato ya kitandani, hata iliwabidi tu kutumia shuka la kuvutwa. Kisha kasema, “Mimi na mke wangu tulienda kule na kubadilisha kitanda chake mara mbili kwa siku.” Kisha kasema, “Daktari alimkatia tamaa yapata majuma sita kabla ya hapo, na kumpa tu fenobito ya kutosha kudumu mpaka atakapoondoka. Ile kansa, walimfanyia upasuaji kisha wakamfunika tu, kwa hiyo, kasema, hakuna haja ya kujipumbaza naye tena.” Kisha kasema, “Nanyi mwajua, alikuwa ameketi hapo akila, kisha akaruka juu, na kukimbia, akatusalimia kwa mkono.” Naye akasema. . .

Nikasema, “Usiseme?”

¹⁵⁰ Kasema, “Naam.” Kasema, “Sasa,” tena kasema, “kama huamini hilo,” kasema, “kwea moja kwa moja kule juu ukaone, yeye mwenyewe atakwambia.” Mnaona, alikuwa akinihubiria tena basi. Nikamwacha ashuhudie kidogo.

Nikasema, “Loo, huamini hilo, sivyo?”

Akasema, “Hakika.” Kasema, “Kama huamini hilo, nenda tu— panda moja kwa moja kule kilimani upate kujua. Nitakupeleka kule juu.”

Nikasema, “Um-hum.” Kasema, “La,” nikasema, “nitaamini usemalo juu yake.” Mnaona? Nikasema, “Nitaamini usemalo juu yake.” Nikasema, “Aisee, jamaa huyo alikuwa ni nani?”

¹⁵¹ “Sijui.” Kasema, “Anatoka huko *Indiana*’r, nao walisema atashuka kuja huku tena.” Kasema, “Nitamwendea atakapokuja.” Kasema, “Nitamwendea na kusema, ‘Ninataka kukwambia jambo fulani, Mhubiri. Niambie jinsi ulivyojua hilo kamwe, wakati hukuwahi kuwa katika nchi hii hapo kabla.’” Sikuwa nimeenda, mnaona. Kasema, “Ilikuwa je, ulijua je hilo?”

Nikasema, “Naam, Bwana. Vema, hakika natumaini utakutana naye.” Nikasema, “Natumaini atakusaidia.”

Naye akasema, “Vema, ninaenda.” Alikuwa akitafuna tumbaku, mwajua, naye akatema chini namna *hiyo*, nayo majani yakaruka.

¹⁵² Nami nikasema, “Nawe unataka kuniambia sasa . . . Turudi kwenye mti huu,” nikasema, “Ni—ninashangazwa na jambo hilo.” Ndipo nikasema, “Unajua, hata hatujawa na usiku baridi, hakuna jalidi wala chochote kile,” Kisha nikasema, “majani hayo yanaanguka ardhini kutoka kwenye mti huo. Na hiyo ndiyo sababu tulikuja huku, tulikuwa tumetoka kwenye hiyo misitu tambarare, ambako majani yanaanguka chini, yanakauka, na kuingia kwenye mabonde haya hapa, ambapo yanaanguka majini na kulowa maji.” Nikasema, “Nawe . . . Kwa nini hayo majani yanaanguka kutoka kwenye mti huo?”

“Vema,” akasema, “uhai uliyaacha.”

Nikasema, “Ati nini?”

Akasema, “Uhai uliyaacha.”

“Uliacha jani?”

“Naam.” Kasema, “Hiyo ndiyo sababu linaanguka.”

Nikasema, “Vema, hatujawa na jalidi yoyote wala dalili yoyote ya hali ya hewa baridi.”

Akasema, “Vema, unayaacha tu.”

Nami nikasema, “Vema, inakuwaje kwa huo uhai?”

Akasema, “Unashuka chini kwenye mzizi wa mti.”

Nikasema, “Unamaanisha nini, ati mzizi?”

Kasema, “Vema, baridi kali ingeugandisha, nayo ingeua hiyo chembechembe ya uhai kwenye mti.”

Basi nikasema, “Halafu unashuka chini kwe—kwenye shina la mti kujificha huko, mpaka lini?”

Akasema, “Mpaka majira ya kuchipua.”

“Kisha unakuletea kichala cha matofaa mengine, na lundo la majani?”

“Naam, Bwana.”

“A-ha,” nikasema, “ajabu hiyo.” Nikasema, “Ni—ningetaka kukuuliza jambo fulani.”

Akasema, “Naam, Bwana.”

¹⁵³ Nikasema, “Ni Akili gani inayouambia mti huo, uhai huo katika mti huo, kwamba majira ya baridi kali yanakuja, na usipotoka kwenye matawi haya na kushuka hapa chini, na kufunikwa na mizizi hii, kwamba utakufa? Nao uhai huo huitii Akili hiyo, na kushuka chini kwenye mzizi wa mti, na kukaa huko chini mpaka majira ya baridi kali yatakapopita, halafu unatoa jani tena.” Nikasema, “Ni Akili gani inayofanya hivyo, Bwana?”

Naye akasema, “Loo, ni maumbile.”

Nikasema, “Maumbile ni nini?”

¹⁵⁴ Akasema, “Vema, kwa kweli hufanya hivyo.” Aliona hoja yangu, mnaona, naye alikuwa akijaribu kujificha kutoka kwake. Naye akasema, “Vema, wewe,” akasema, “unaona . . .”

¹⁵⁵ Nikasema, “Vema, hebu nikwambie, hebu tuchukue ndoo ya maji, na kuiweka hapa nje kwenye ile nguzo ya mwaloni, na sasa, katikati ya Agosti, yatashuka chini ya hiyo nguzo, na kukaa huko mpaka majira ya kuchipua, kisha yarudi na kuijaza hiyo ndoo tena. Yatafanya hivyo?”

Akasema, “La, la.”

¹⁵⁶ Basi nikasema, “Vema, niambie ni Akili gani. Haina budi kuwa ni Akili sasa, kwa sababu huo mti hauna Akili. Haina budi kuwa ni Akili ya kufanya uhai huo utoke kwenye huu mti hapa juu kwenye matawi hadi mizizini, na Akili ya kuuambia ni wakati wa kurudi juu tena.”

Akasema, “Kamwe sikuwa nimewazia hilo.”

¹⁵⁷ Nami nikasema, “Sasa, liwazie hilo kwa muda mrefu, na utakapojua ni Akili gani hiyo iliyoambia . . . inayouambia huo utomvu mtini, huo uhai, kushuka chini mizizini na kujificha la sivyoy utakufa, basi nitakwambia ile Akili iliyoniambia mwanamke huyo alikuwa ni nani na jambo la kufanya ili kuyaokoa maisha yake.”

Akasema, “Wewe siye huyo mhubiri!”

Nikasema, “Ndimi.”

¹⁵⁸ Hapo, “Nionyeshe. Wewe utanionyesha njia ya Uzima,” ingawa ni rahisi sana. Na hapo, akapiga magoti, huku amevua kofia yake, nikamwongoza kwa Kristo. “Nionyeshe njia Yako ya Uzima,” kwa mkulima asiye na elimu, ambaye labda asingeweza kuandika jina lake mwenyewe, bali Mungu anayo njia ya kuchukua njia ya Uzima, kumwongoza kwenye Hiyo.

¹⁵⁹ Basi, ndugu, tunaning’inia kwenye Mti wa Uzima, na siku moja jani hili kuukuu litaanguka, bali kutakuja ufufuo siku moja, Utawala mkuu wa Miaka Elfu umewekwa mbele zetu, ufufuo mkuu. Tutarudi tena siku moja, kwa sababu tunao Uzima wa Milele, tunaelewa hilo kwa njia ya Neno. Kama tungalikuwa na wakati, mwajua, jinsi ulivyo, tungeweza kuuendea kwa njia nyingi. Enyi watu, wakati mwingine inakubidi kutumia njia mbalimbali kumfikia mtu.

¹⁶⁰ Mwaka jana nilishuka nikaenda kule, nikawaza, “Nitaenda kuwinda kwa yule mzee tena.” Nikaendesha gari mpaka huko, nayo magugu yalikuwa yameotea pande zote, nikamwona mama mkongwe ameketi barazani, akimenya matofaa kutoka kwenye mti ule ule. Nikaenda pale, nikasema, “U hali gani?”

Akasema, “Njema, Bwana?”

Nami nikasema. . . Nilikuwa nimeona mabango makubwa yaliyobandikwa kila mahali kabla sijaingia mle. Nami nikasema, “Sijui kama ingewezekana niwinda kuchakulo.”

¹⁶¹ Akasema, “Bwana, wakati mume wangu alipokuwa hai, alikuwa wa kipekee sana, aliweka masharti.” Kisha kasema, “Nina wavulana kutoka. . . wanaishi huko Kentucky, huko Louisville, Kentucky,” kasema, “nao wanashuka kuja kuwinda.”

Nikasema, “Nilifahamu hilo, aliniambia hivyo. Ninaweza kumwona?”

Akasema, “Ametuacha.”

Nikasema, “Usiseme.”

“Ndiyo.”

Nikasema, “Vema, aliniambia, wakati alipokuwa hai, kwamba ningeweza kuwinda.”

Akasema, “U nani wewe?”

Nikasema, “Mimi ni Ndugu Branham.”

¹⁶² Akaangusha sufuria yake, akanishika mkono, akasema, “Ndugu Branham, yeye yuko Utukufuni sasa.” Akasema, “Aliishi maisha thabiti ya Kikristo tangu wakati huo.”

¹⁶³ Nikasema, “Nawe unamenya matofaa kutoka kwenye mti uo huo.” Nikasema, “Matofaa yalirudi tena, sivyo?” Nikasema, “Ndivyo atakavyofanya wakati mwingine, katika ule ufufuo mkuu.”

¹⁶⁴ Basi, ndugu, dada, hatuwezi kuwaruhusu watu tunaowapenda, na ambao Kristo aliwafia, wauache Uzima

huu, kufa bila Uzima wa Milele. Hebu na tufanye yote tuwezayo kuwaingiza mahali hapo ambapo wanaweza kufufuka tena katika ule ufufuo. “Utanionyesha njia ya Uzima.”

¹⁶⁵ Ninyi ndugu mnaweza kufanya hivyo kwa makusanyiko yenu, kwa sababu ninyi, wengi wenu ni wahudumu wenye elimu na wanatheolojia. Si—sina uwezo huo. Lakini maskini ninii yangu. . . Sina uwezo, bali ka—karama ndogo niliyopewa, kama kujiingiza kwenye gia *fulani*, ambapo watu, yale wanayowazia, yale wanayofanya, na kile kinachopaswa kufanywa, hiyo ndiyo njia ndogo ya huduma yangu. Ni mojawapo tu ya njia ndogo ambazo Mungu huniruhusu kutumia ku—kuwaleta watoto Wake Upande ule.

Nami ninaunganisha yangu na zenu, sasa. Basi hima tuwaonyeshe watu njia ya Uzima, wapate kuiona njia ya Bwana.

¹⁶⁶ Na ninii. . . Yeye alisema hapa, “Kwa maana kuna furaha Mbele za Mungu.” Kuna furaha, tunapotembea kwenye njia hii, tukiangalia huku na huko, ufufuo wa miti, majani, kila kitu, hunena juu ya Mungu. Kwa hiyo hebu na tuwe kama viumbe vya Mungu, tukinena habari za Mungu katika kila kitu tufanyacho ama—ama kusema, na liangaze kwa utukufu Wake. Mungu awabariki. Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu sasa.

¹⁶⁷ Bwana Yesu, Mchungaji Mkuu wa kundi, nina furaha sana, Bwana, kwamba Wewe ulinionyesha njia ya Uzima. Nami nina furaha sana kutembea kwenye barabara hii kuu ya kale, ninashukuru sana kuunganisha mikono yangu na ndugu hawa leo, tunaposimama kando ya barabara kuu, tukipiga mayowe kwa sauti zetu, na talanta zote ambazo umetupatia kwa umati huo unaokufa wa wanadamu huko nje ambao uliufia Wewe. Bwana, tusaidie, utatusaidia tafadhali?

¹⁶⁸ Jalia kila moja ya maisha yetu yawe mti, ama kitu fulani ambacho kitaleta imani kuu sana kwa mwenye dhambi na asiyeamini, hata watu, waweze kuiona njia ya Bwana na kuingia katika furaha za Bwana. Tujalie, Baba. Tubariki katika jitihada zetu dhaifu pamoja.

¹⁶⁹ Tunakushukuru kwa ajili ya wakati huu mzuri sana wa ushirika, kiamshakinywa hiki kizuri sana. Na, Baba, tunajisikia ya kwamba tuna ninii tu. . . Nafsi zetu na miili yetu inalishwa na wema wa Mungu.


¹⁷⁰ Kuwa pamoja nasi, sasa, tunapoendelea mbele zaidi kuingia katika mikutano mingine zaidi, na uwe pamoja nasi usiku wa leo, na jalia jambo fulani lifanyike ambalo litawafanya wenye dhambi waje upesi madhabahuni wapate kuokolewa. Jalia wagonjwa waponywe, na wale wasio na Roho Mtakatifu, jalia wabatizwe katika Mwili wa Kristo. Tujalie, Bwana.

¹⁷¹ Tunajikabidhi Kwako. Tunayachukua maombi yetu, imani yetu, na tunayaweka pamoja, tunayaweka juu ya madhabahu

Yako, nasi tunayatuma Kwako, Bwana. Katika Jina la Yesu Kristo, tupokee. Amina.

¹⁷² Mungu awabariki, ndugu zangu. Nami nadhani sasa, mmoja wa hao ndugu atakuja kwa ajili ya kuliachilia kanisa, ama, kukusanyiko, rasmi, jinsi ipaswavyo.

¹⁷³ Na wakati wakiamua ni nani anayekuja, ninataka kusema, ninawashukuru kwa mahudhurio yenu mema, na ninasikitika nimewaweka hapa kufikia adhuhuri kabisa, karibu dakika tano baada ya saa tano kwa saa yangu hapa. Nami ningeweza tu kuketi na kuzungumza nanyi kuhusu mambo makuu ambayo nimeona yakitukia, anayofanya Bwana katika huduma za kimishenari, na mambo ya jambo kuu, kuu sana. Kamwe msio gope. Kumbukeni tu, Mungu aliahidi, Mungu hana budi kutimiza ahadi Yake, hana budi kuitimiza tu ahadi Yake.

Mungu awabariki sasa. Ndugu Borders. 

62-0621B Njia Ya Uzima
First Hebrew Christian Synagogue
Los Angeles, California Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org